**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**
**WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI**

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 ILIYOWASILISHWA NA MHESHIMIWA DKT. KHALID SALUM MOHAMED (MBM) WAZIRI WA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI.

**KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MEI, 2024**



*Muonekano wa Daraja la juu (Fly Over) katika eneo la Mwanakwereke baada kukamilka Ujenzi huo*

## VIONGOZI WA WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI - ZANZIBAR



**Mhe. Dk. Khalid Salum Mohamed (MBM)**
**Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi**
**Zanzibar**



**Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Alwardy**
**Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi**
**Zanzibar**



**Dkt. Mngereza Mzee Miraji**
**Katibu Mkuu -WUMU**
**Zanzibar**



**Nd. Makame M. Haji**
**Naibu Katibu Mkuu – Ujenzi na Uchukuzi**
**WUMU – Zanzibar.**



**Dkt. Mzee S. Mndewa**
**Naibu Katibu Mkuu – Mawasiliano**
**WUMU – Zanzibar.**



**Nd. Ibrahim Salehe Juma**
**Afisa Mdhamini**
**WUMU – PEMBA**

**YALIYOMO**

YALIYOMO ........................................................................................ ii
ORODHA YA VIAMBATANISHO ............................................................ v
A. UTANGULIZI ................................................................................. 1
B. MAJUKUMU NA MUUNDO WA WIZARA .............................................. 3

C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI, 2023 HADI MACHI, 2024 ................................................................ 3
C.1. Ukusanyaji wa Mapato kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 ................................................................................ 3
C.2. Fedha zilizopatikana kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024....... 4
C.3. Utekelezaji wa Programu za Wizara kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 ................................................................ 4

C.3.1. PROGRAMU YA USAFIRISHAJI ................................................... 5
C.3.1.1. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji ................................................................ 5

C.3.2. PROGRAMU YA UJENZI NA MAJENGO YA SERIKALI ....................... 20
C.3.2.1. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Ujenzi na Majengo ya Serikali 20

C.3.3 PROGRAMU YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA) ................................................................ 25
C.3.3.1. Programu Ndogo ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA......... 25

C.3.4. PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA ............... 28
C.3.4.1. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji.......... 28
C.3.4.2. Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara ................................................................ 30
C.3.4.3. Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba......... 32

D. UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 HADI MACHI 2024 PAMOJA NA MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 ................................................ .33

D.1 MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI ZANZIBAR ........33
D.2 MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI ZANZIBAR.................................37
D.3 MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR .............................41
D.4 SHIRIKA LA BANDARI ZANZIBAR.................................................47
D.5 SHIRIKA LA MELI ZANZIBAR.......................................................56
D.6 SHIRIKA LA MAWASILIANO ZANZIBAR .......................................58
D.7 BODI YA USAJILI WASANIFU, WAHANDISI NA WAKADIRIAJI MAJENGO ZANZBAR.......................................................................63
D.8 BODI YA USAJILI WA WAKANDARASI ZANZIBAR ............................64

E. MASHIRIKIANO NA TAASISI ZA MUUNGANO ...................................64
F. MCHANGO WA SEKTA BINAFSI KATIKA SEKTA YA UJENZI, USAFIRISHAJI NA MAWASILIANO ............................................................................ 65

G.MUELEKEO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI KWA KILA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025.............66

G.1. VIPAUMBELE VIKUU VYA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025...........................................................................................66

G.2. MUHTASARI WA MAELEZO KWA KILA PROGRAMU NA MALENGO YANAYOTARAJIWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 ..........................................................................................67

G.2.1 PROGRAMU YA USAFIRISHAJI..................................................67
G.2.1.1 Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji. ..........................................................................67

G.2.2. PROGRAMU YA UJENZI NA MAJENGO YA SERIKALI....................70
G.2.2.1. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Ujenzi na Majengo ya Serikali...........................................................................................71

G.2.3 PROGRAMU YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA) ..................................................................................72
G.2.3.1 Programu Ndogo ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA........72

G.2.4 PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA ............... 73
G.2.4.1 Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji ......... 73
G.2.4.2 Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara ................................................................................ 74
G.2.4.3 Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba ........ 75

H.HITIMISHO................................................................................ 76

I. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 .................. 79

## ORODHA YA VIAMBATANISHO


**Kiambatanisho Nambari 1A.**Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa programu kwa Kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024..81

**Kiambatanisho Nambari 1B:** Fedha zilizopatikana kwa Kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 ........................................................... 82

**Kiambatanisho Nambari 2.** Matengenezo ya Vyombo vya moto kwa Kipindicha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 ..............................................82

**Kiambatanisho Nambari 3A:** Orodha ya Barabara zilizofanyiwa usafi wa ukataji majani, Usafishaji wa misingi na makalvati Unguja na Pemba .83

**Kiambatanisho Nambari 3B:** Orodha ya Barabara zilizofanyiwa matengenezo ya kawaida ya uzibaji mashimo. .................................... 85

**Kiambatanisho Nambari 4:** Orodha ya Barabara za Mji ni zenye urefu wa Kilomita 100.9zinazoendelea kujengwa Unguja............................... 86

**Kiambatanisho Nambari 5:** Orodha ya Barabara za ndani zenye urefu wa Kilomita 275.9 zinazoendelea kujengwa Unguja na Pemba ............. 89

**Kiambatanisho Nambari 6A :** Nyaraka za Ujenzi zilizotayarishwa kwa Kipindi cha Julai 2023 hadi Machi, 2024 ..............................................92

**Kiambatanisho Nambari 6B :** Utekelezaji wa kazi za usimamizi wa ujenzi kwa kipindi Julai, 2023 hadi Machi, 2024 ....................................94

**Kiambatanisho Nambari 7A:** Maeneo yaliyojengwa Minara ya Mawasilianokwa Unguja na Pemba kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024......................................................................................98

**Kiambatanisho Nambari 7B**: Hali ya upatikanaji wa Mawasiliano katika Visiwa vidogo vidogo ...............................................................98

**Kiambatanisho Nambari 8A:** Wafanyakazi waliopatiwa Mafunzo ya Muda Mrefu kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 .................... 100

**Kiambatanisho Nambari 8B:** Wafanyakazi waliopatiwa Mafunzo ya Muda Mfupi kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024..................... 100

**Kiambatanisho Nambari 9A:** Ukaguzi wa Vyombo vya Moto kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024....................................................... 100

**Kiambatanisho Nambari 9B:** Utoaji wa Ruhusa za Njia na Usafirishaji kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024...................................... 101

**Kiambatanisho Nambari 9C:** Utoaji wa Beji za Utingo na Madereva kwa Kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 ........................................... 101

**Kiambatanisho Nambari 10A:** Idadi ya Ndege zilizohudumiwa kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024. .......................................... 102

**Kiambatanisho Nambari 10B:** Kampuni za Ndege zilizotumia Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 .......................................................................... 102

**Kiambatanisho Nambari 10C:** Idadi ya Abiria waliohudumiwa kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 ............................................ 106

**Kiambatanisho Nambari 11.** Kazi za matengenezo ya Barabara zilizopangwa kufanyika kwa mwaka wa fedha 2024/2025 .................... 106.

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu lipokee, lizingatie, lijadili na hatimae likae kama kamati ili liweze kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa kazi za kawaida na kazi za Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

2. **Mheshimiwa Spika,** nianze kwa kumshukuru Allah (S.W) kwa kutujaalia uhai na afya njema na kutuwezesha kushiriki katika kikao hiki cha Baraza la Wawakilishi kinachojadili Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ikiwa leo hii tunajadili utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na Mwelekeo wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

3. **Mheshimiwa Spika,** kwa dhati kabisa nachukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuiongoza vyema Zanzibar kwa kuwaletea maendeleo wananchi wake. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa Maelekezo na Miongozo anayoitoa kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi katika kuendeleza Sekta za Ujenzi, Usafirishaji na Mawasiliano. Maelekezo na miongozo anayoitoa Mheshimiwa Rais inatusaidia sana kuongeza ufanisi wa kazi na kasi ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii. Kwa hakika chini ya Uongozi wake, Mheshimiwa Rais ametekeleza kwa vitendo ahadi alizozitoa kwa wananchi wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025. Kipekee kabisa, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuiongoza vyema Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa lengo la kuleta maridhiano na kuwaunganisha Wazanzibari wote pamoja na kuhakikisha amani, utulivu na mshikamano wa Taifa unaendelea kudumu katika nchi yetu.

4. **Mheshimiwa Spika**, vilevile nachukua fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa namna ambavyo wamekuwa wakimsaidia Mheshimiwa

Rais katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Nawashukuru viongozi wetu hawa kwa miongozo wanayotupatia katika Wizara yetu ambayo imetuwezesha kutekeleza kazi zetu za Wizara kwa ufanisi, uwazi na umakini. Aidha, naomba kumpongeza tena Makamu wa Pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, kwa kusimamia vyema shughuli za Serikali pamoja na kuratibu vizuri shughuli zote za Baraza lako Tukufu.

5. **Mheshimiwa Spika,** namshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Dkt. Mwinyi Talib Haji pamoja na watendaji wake kwa mashirikiano yao makubwa wanayotupatia katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii.

6. **Mheshimiwa Spika,** napenda pia nikupongeze wewe binafsi kwa umahiri, hekima na busara unazozitumia katika kuliongoza Baraza letu la Wawakilishi. Aidha, pongezi hizi ziende pia kwa Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Baraza pamoja na Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kusaidia kuendesha shughuli za Baraza hili.

7. **Mheshimiwa Spika,** kwa mapenzi makubwa sana natoa shukurani zangu kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati chini ya uongozi makini wa Mwenyekiti wake Mheshimiwa Yahya Rashid Abdalla, Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Kwahani kwa maoni, hoja, mapendekezo, ushauri na maelekezo ambayo yanaisaidia sana Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi katika utekelezaji wa majukumu yake. Kamati hii ilipata nafasi ya kutembelea Taasisi na miradi mbalimbali iliyomo ndani ya Wizara hii na kutoa ushauri na maoni yenye lengo la kuimarisha utekelezaji wa miradi hiyo. Ushauri, maoni na maelekezo hayo, yataendelea kuzingatiwa kwa vitendo wakati wa utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

## B. MAJUKUMU NA MUUNDO WA WIZARA

8. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ina jukumu la kusimamia Sekta ya Ujenzi, Usafirishaji na Mawasiliano. Wizara inatekeleza majukumu hayo kupitia idara tatu (3), Ofisi kuu Pemba na Taasisi kumi na moja (11) zinazojitegemea zinazounda Wizara hii. Idara hizo ni:- Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Mawasiliano Taasisi zinazojitegemea ni:- Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani, Mamlaka ya Usafiri Baharini, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, Shirika la Bandari, Shirika la Meli, Shirika la Mawasiliano, Wakala wa Barabara, Wakala wa Karakana Kuu ya Magari, Wakala wa Majengo, Bodi ya Usajili Wakandarasi pamoja na Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo.

## C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI, 2023 – MACHI, 2024

### C.1. Ukusanyaji wa Mapato kwa Kipindi cha Julai 2023 hadi Machi, 2024

9. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ilikadiria kukusanya jumla ya **TSH 105,000,000** na kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 ilikadiria kukusanya jumla ya **TSH 76,000,000.** Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **TSH 86,574,171** zimekusanywa sawa na asilimia 113.9 ya makadirio kwa kipindi hicho ambapo ni sawa na asilimia 82.4 kwa makadirio ya mwaka. Aidha, Wizara ilipokea makusanyo ya **TSH 1,242,988,757** kutoka kwa Taasisi zetu za Wakala wa Majengo, Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo na Bodi ya Usajili Wakandarasi zilizohamishiwa kutoka Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Zanzibar mwezi wa Septemba, 2023. Uhamisho huu ulitokana na mabadiliko ya taasisi za Serikali ya kuziondoa taasisi za ujenzi kutoka Wizara ya Ardhi na kuzileta katika Wizara ya Ujenzi kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wa Wizara hizi.

## C.2. Fedha zilizopatikana kwa Kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024

10. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kupitia Programu zake kuu tatu (3) kwa mwaka wa fedha 2023/2024, iliidhinishiwa na Baraza la Wawakilishi kutumia jumla ya **TSH 571,490,700,000.** Kati ya fedha hizo **TSH 2,751,300,000** ni mshahara, **TSH 2,630,700,000** kwa kazi za kawaida, **TSH 6,661,700,000** ni Ruzuku na **TSH 559,447,000,000** kwa kazi za maendeleo.

    Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 Wizara ilipanga kutumia jumla ya **TSH 474,127,122,680**. Kati ya fedha hizo **TSH 2,210,768,103** kwa kazi za kawaida, **TSH 2,063,475,749** ni mshahara, **TSH 5,292,878,828** ni ruzuku na **TSH 464,560,000,000** kwa kazi za maendeleo.

11. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya **TSH 355,781,992,021.79** zimepatikana sawa na **asilimia 75** ya makadirio ya bajeti kwa kipindi cha miezi tisa na **asilimia 62.2** kwa makadirio kwa mwaka. Kati ya fedha hizo, **TSH 346,213,744,114.4** ni kwa kazi za maendeleo sawa na **asilimia 74.5** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 61.8 ya makadirio ya mwaka, **TSH 3,008,056,086** ni mshahara sawa na **asilimia 145.7** ya makadirio ya miezi tisa na **asilimia 109.3** kwa mwaka, **TSH 1,248,363,100** ni kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 56.5 ya makadirio ya miezi tisa na **asilimia 47** ya makadirio ya mwaka na TSH 5,311,828,721.39 ni Ruzuku kwa taasisi zilizomo ndani ya Wizara sawa na **asilimia 100.3** ya makadirio ya miezi tisa na **asilimia 79.7** ya mwaka. **Kiambatanisho namba 1A na 1B kinatoa ufafanuzi**.

## C.3. Utekelezaji wa Programu za Wizara kwa Kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024

12. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha, 2023/2024, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi imetekeleza kazi zake kupitia Programu kuu nne (4) na Programu ndogo sita (6), Utekelezaji wa programu hizo kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 ni kama ifuatavyo: -

### C.3.1. PROGRAMU YA USAFIRISHAJI

**13. Mheshimiwa Spika,** programu hii ina lengo la kuimarisha miundombinu na huduma za usafiri zilizo bora, salama na endelevu na zitakazoleta matokeo bora katika program ya usafirishaji. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu ya Usafirishaji ina Programu ndogo moja (1) ambayo ni Programu ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji.

#### C.3.1.1. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji.

**14. Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Idara moja (1) na Taasisi mbili (2) zinazojitegemea ambazo ni Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Wakala wa Karakana Kuu ya Magari pamoja na Wakala wa Barabara. Wizara kupitia programu hii imetekeleza mambo yafuatayo:-

### WAKALA WA KARAKANA KUU YA MAGARI ZANZIBAR

15. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Karakana Kuu ya Magari kupitia programu ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji imepewa jukumu la kuvifanyia matengenezo vyombo vya moto vya Serikali na binafsi kupitia Karakana zake zilizopo Unguja na Pemba pamoja na kutoa ushauri wa ununuzi na uuzaji wa gari za Serikali.

**16. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kupitia Wakala wa Karakana Kuu ya Magari imefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo: -

a. **Matengenezo ya Vyombo vya Moto (Gari) vya Serikali na Binafsi:** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wakala wa Karakana Kuu ya Magari ilikadiria kufanya matengenezo ya vyombo vya moto 2,080 vya Serikali na Binafsi kwa Unguja na Pemba, na kwa kipindi cha miezi tisa kutoka Julai, 2023 hadi Machi, 2024 Wakala ilikadiria kufanya matengenezo ya gari 1,560 ambapo, hadi kufikia Machi 2024 jumla ya vyombo vya moto 1,370 vimefanyiwa matengenezo Unguja na Pemba sawa na asilimia 87.8 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 65.8 ya makadi-

rio ya mwaka.  Kati ya gari hizo, 1,272 ni za Serikali na 98 ni gari za watu binafsi. Aidha, jumla ya gari 1,254 zimefanyiwa matengenezo Unguja na gari 116 zimefanyiwa matengenezo Pemba.  Kiambatanisho Nambari 2 kinahusika.

b. **Kuimarisha huduma za matengenezo ya Magari,** katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za matengenezo ya magari na vyombo vya moto katika Karakana zote za Serikali kwa ufanisi, Wakala wa Karakana Kuu ya Magari imefanikiwa kununuwa vifaa mbalimbali kwa ajili ya matengenezo ya magari ikiwemo vipuri na vilainishi pamoja na kuwapatia mafundi mafunzo ya muda mfupi kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa karakana zetu za Unguja na Pemba.

c. **Utoaji wa Ushauri wa Kitaalamu Juu ya Ununuzi na Uuzaji wa Vyombo vya Moto vya Serikali:** Wakala wa Karakana Kuu ya Magari inaendelea kutoa ushauri wa kitaalamu kabla ya ununuzi wa vyombo vya moto pamoja na kuvihakiki baada ya ununuzi. Kwa mwaka wa fedha, 2023/2024 ilikadiria kutoa ushauri wa kitaalamu kwa taasisi 32 na hadi kufikia Machi, 2024 imefanikiwa kutoa ushauri wa kitaalamu kwa taasisi 13 za Serikali sawa na asilimia 40.6 ya makadirio ya  mwaka. Aidha, Wakala ilikadiria kufanya ukaguzi wa vyombo vipya 94 ambapo imefanikiwa kukagua jumla ya vyombo vipya 79 kutoka taasisi mbali mbali sawa na asilimia 84 ya makadirio ya mwaka.

d. **Uimarishaji wa Ofisi na Karakana Unguja na Pemba:** Katika kuimarisha utoaji wa huduma bora za Kiutawala na Kiufundi kwa wakati, Wakala imeimarisha vitendea kazi ikiwemo kuvifanyia matengenezo vyombo vya usafiri, upatikanaji wa huduma ya mtandao (LAN na INTERNET) na ununuzi wa vipuri. Aidha, Karakana imewapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi watano (5) ambao ni sawa na asilimia 71.4 ya makadirio ya wafanyakazi saba (7) waliopangwa kupatiwa mafunzo kwa mwaka 2023/2024. Pia, Wakala imefanikiwa kusaini Hati ya makubaliano ya kisheria "Memorandum of Understanding" (MOU) yanayoainisha maeneo ya mashirikiano baina ya Wakala wa Karakana na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) ya SJMT.

**Mapato na Matumizi**

17. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar ilikadiria kukusanya jumla ya **TSH 105,000,000** na kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, ilikadiria kukusanya jumla ya **TSH 76,000,000** na hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **TSH 86,574,171** zimekusanywa sawa na **asilimia 113.9** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **82.4** ya makadirio ya mwaka. Aidha jumla ya **TSH 69,385,276** zimekusanywa Unguja na **TSH 17,188,895** zimekusanywa Pemba.

18. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wakala wa Karakana Kuu ya Magari ilipangiwa kutumia jumla ya **TSH 1,445,230,000** ikiwa ni ruzuku kwa kazi za kawaida na Mshahara. Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 ilipangiwa kutumia jumla ya **TSH 1,331,204,910**. Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya **TSH 1,421,031,010** zimetumika sawa na **asilimia 106.7** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 98.3 kwa makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, **TSH 1,080,270,910** ni Mshahara na **TSH 340,760,100** ni matumizi ya kawaida.

**WAKALA WA BARABARA ZANZIBAR**

19. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Barabara Zanzibar kupitia Programu ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji ina jukumu la kujenga, kutunza na kuzifanyia matengenezo barabara mbalimbali za Unguja na Pemba ili ziweze kupitika kwa usalama muda wote. Aidha, Wakala wa Barabara Zanzibar ina jukumu la kutoa huduma za usimamizi na ushauri wa kitaalamu kwa miradi ya barabara.

20. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kupitia Wakala wa Barabara Zanzibar kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 imefanikiwa kuzifanyia matengenezo barabara pamoja na miundombinu ya maji ya mvua kwa Unguja na Pemba kama ifuatavyo:-

a. **Ujenzi wa Msingi wa Maji ya Mvua Eneo la Mfenesini Unguja Awamu ya Pili (mita 500):** Wakala wa Barabara Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ilipanga kuendelea na ujenzi wa msingi wa maji ya mvua eneo la Mfenesini kwa awamu ya pili wenye urefu wa mita 500 pamoja na vivuko viwili. Kazi za ujenzi zinatekelezwa na Kampuni ya Lukolo kutoka Dar es Salam chini ya usimamizi wa Wakala wa Barabara Zanzibar kwa gharama ya **TSH. 2,273,458,046** na kazi za ujenzi zimeanza na zitachukuwa muda wa miezi sita hadi kukamilika kwake. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya **TSH 2,353,200,000** na hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya **TSH 470,640,000** zimepatikana sawa na asilimia 20 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, **TSH 341,018,706.9** zimetumika kwa ajili ya kumlipa Mkandarasi ikiwa ni malipo ya awali.

b. **Ujenzi wa Barabara ya Mshelishelini – Bandamaji (1.2km) kwa kiwango cha kifusi Awamu ya kwanza:** Wakala wa Barabara Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ilipanga kujenga barabara ya Mshelishelini – Bandamaji yenye urefu wa kilomita 1.2 kwa kiwango cha kifusi awamu ya kwanza. Kazi za ujenzi wa Barabara hii zinatekelezwa na Mkandarasi Kampuni ya OCRA kutoka Dar es Salaam na ikisimamiwa na Wakala wa Barabara Zanzibar. Muda wa utekelezaji wa mradi huu ni miezi sita (6). Hadi kufikia Machi 2024, kazi iliyofanyika ni kusainiwa Mkataba wa Ujenzi na Mkandarasi na kazi za ujenzi zinatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi wa Mei, 2024. Kwa mwaka wa fedha, 2023/2024, Ujenzi wa barabara hii ulipangiwa kutumia jumla ya **TSH 420,000,000** na hadi kufikia Machi 2024 jumla ya **TSH 294,000,000** zimepatikana sawa na asilimia 70 ya makadirio ya mwaka.

c. **Ujenzi wa Barabara zinazounganisha Miradi ya UVIKO19 Unguja:** Wakala wa Barabara Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2023/2024, ilipanga kujenga jumla ya kilomita 0.85 za barabara zinazounganisha miradi ya UVIKO19 kwa upande wa Unguja. Barabara hizo ni Kitogani Hospitali ya Wilaya ( 0.12km), Shule ya msingi ya Mama Samia Suluhu - Mwanakwerekwe ( 0.13km), Soko la Wajasiriamali la Hanyegwa Mchana ( 0.12km), Soko la Wajasiriamali

la Kinduni ( 0.06km), Kivunge Hospitali ya Wilaya ( 0.3km) na Soko la Wajasiriamali la Pale ( 0.12km). Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, jumla ya kilomita kilomita 0.25 zilijengwa kwa kiwango cha lami ngumu na kilomita 0.6 kwa lami ya maji. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, ujenzi wa barabara hizi ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 58,800,000 na zimepatikana na kutumika.

d. **Ujenzi wa Barabara ya Mgelema - Wambaa 5.85 kmkwa Kiwango cha Lami:** Ujenzi wa barabara hii ni mwendelezo wa ujenzi wa barabara ya Kipapo - Mgelema - Wambaa yenye urefu wa 9.4 km, ambapo kilomita 5.3 zimekamilika kwa kiwango cha lami. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, jumla ya kilomita 4.1ambazo zilipangwa kujengwa kwa kiwango cha lami kutoka Mgelema hadi Wambaa zikijumuisha barabara za ndani zinazounganisha na barabara hiyo zenye urefu wa kilomita 1.75. Hivyo barabara ya Kipapo - Mgelema hadi Wambaa itakuwa na urefu wa kilomita 11.15 hadi kukamilika kwake. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya kilomita 3 zimejengwa kwa kuwekewa matabaka tofauti ya kifusi (G7 na G15) ambapo kazi hiyo ni sawa na asilimia 30 ya utekelezaji wa ujenzi wa barabara hiyo. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 620,496,000 na hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya **TSH 496,000,000** zimepatikana sawa na **asilimia 79.9** ya makadirio.

e. **Ujenzi wa Barabara ya ndani Tunguu (1.1km) kwa Kiwango cha Lami - Unguja:** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wakala wa Barabara Zanzibar ulipanga kujenga barabara ya ndani eneo la Tunguu yenye urefu wa kilomita 1.10 kwa kiwango cha lami. Kazi za ujenzi zimekamilika kwa hatua za kifusi na zinatekelezwa na Wakala wa Barabara Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, ujenzi wa barabara hii ulipangiwa kutumia jumla ya **TSH 130,000,000** na hadi kufikia Machi, 2024 jumla **TSH 75,000,000** zimepatikana sawa na **asilimia 57.7** ya makadirio.

f. **Ujenzi wa Barabara Kwenye Kiwanja cha Maonesho ya siku ya Wakulima (Nane-Nane) - 3.2 km kwa Kiwango cha Lami - Unguja.** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wakala wa Barabara Zanzibar ulipanga kujenga barabara zenye jumla ya kilomita 3.2 kwenye kiwanja cha maonesho ya siku ya wakulima (nane nane) kilichopo Dole (Wilaya ya Magharibi "A") kwa kiwango cha lami. Ujenzi wa barabara hizo unatekelezwa na Wakala wa Barabara Zanzibar na umepangwa kukamilika kwa kipindi cha miezi sita (6) kuanzia mwezi Machi 2024. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya kilomita 3.2 zimesafishwa na kilomita 2.5 zilijengwa kwa tabaka la kwanza la kifusi (G25) sawa na asilimia 30 ya utekelezaji wa mradi huo. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, ujenzi wa barabara hii ulipangiwa kutumia jumla ya **TSH 800,000,000** na hadi kufikia Machi, 2024 jumla **TSH 626,000,000** zimepatikana sawa na **asilimia 78.3** ya makadirio.

g. **Ujenzi wa Barabara ya Ndani yenye Urefu wa Kilomita 4.3 kwa Kiwango cha Kifusi - Pemba:** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wakala wa Barabara ulipanga kujenga barabara za ndani zenye jumla ya urefu wa kilomita 4.3 kwa kiwango cha kifusi. Barabara hizo ni Kuyuni - Kalani (2.5km), Minazini - Shikazako (0.5km), Mauani – Kisimani - Kajirambeni (1.3km) na ujenzi wa kalvati moja. Ujenzi wa barabara hizi unatekelezwa na Wakala wa Barabara na hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya kilomita 3.8 zimekamilika ambazo ni sawa na asilimia 88 ya utekelezaji wa ujenzi wa barabara zote. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Ujenzi huu ulipangiwa kutumia jumla ya **TSH 1,221,000,000** na hadi kufikia Machi, 2024 jumla **TSH 1,221,000,000** zimepatikana sawa na asilimia 100 ya makadirio ya bajeti.

h. **Ujenzi wa Misingi ya Maji ya Mvua Barabara ya Ole - Kengeja 4.9km Awamu ya Kwanza - Pemba:** Wakala wa Barabara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ilipanga kujenga misingi ya maji ya mvua yenye urefu wa kilomita 4.9 awamu ya kwanza na kazi za ujenzi zinatekelezwa na Mkandarasi Kampuni ya Talib Moh'd Said General Supplier kutoka Pemba chini ya Usimamizi wa Wakala wa Barabara Zanzibar. Muda wa ujenzi ni miezi mitatu (3) na hadi kufikia Machi

2024, jumla ya kilomita 4 zimekamilika sawa asilimia 81.6 ya utekelezaji. Kwa mwaka wa fedha, 2023/2024 Ujenzi huu ulipangiwa kutumia jumla ya **TSH 683,000,000** na hadi kufikia Machi 2024, jumla ya **TSH 550,000,000** zilipatikana sawa na asilimia 80.5 ya makadirio ya bajeti.

i. **Ujenzi wa Misingi ya Maji ya Mvua Barabara ya Mtoni Kidatu - Garagara (3 km) Unguja:** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wakala wa Barabara ulipanga kujenga misingi ya maji ya mvua kwenye barabara ya Mtoni Kidatu – Garagara yenye urefu wa kilomita 3. Ujenzi huu unatekelezwa na Mkandarasi kampuni ya OCRA kutoka Dar es Salaam na unasimamiwa na Wakala wa Barabara na muda wa utekelezaji ni miezi sita (6). Hadi kufikia Machi 2024, kazi iliyofanyika ni kusaini Mkataba wa ujenzi na Mkandarasi na kazi za Ujenzi zinatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi wa Mei, 2024. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Ujenzi huu ulipangiwa kutumia jumla ya **TSH 350,000,000** na hadi kufikia Machi 2024, jumla ya **TSH 210,000,000** zimepatikana sawa na **asilimia 60** ya makadirio ya mwaka.

j. **Ujenzi wa Misingi ya Maji ya Mvua Barabara ya Kipapo - Mgelema (3.3km) Pemba:** Kwa mwaka 2023/2024, Wakala wa Barabara Zanzibar ilipanga kujenga misingi ya maji ya mvua katika barabara ya Kipapo – Mgelema yenye urefu wa kilomita 3.3. Kazi za Ujenzi zitafanywa na Kampuni ya ZECCON Co Ltd kutoka Pemba na kusimamiwa na Wakala wa Barabara. Muda wa ujenzi ni miezi mitatu (3) na hadi kufika Machi, 2024 taratibu za Mkataba zimekamilika na utekelezaji wa ujenzi huo utaanza mara tu baada ya kusaini mkataba. Kwa mwaka wa fedha, 2023/2024 Ujenzi huu ulipangiwa kutumia jumla ya **TSH 400,000,000**, na hadi kufikia Machi 2024, jumla ya **TSH 279,000,000** zimepatikana sawa na **asilimia 69.8** ya makadirio ya mwaka.

k. **Ujenzi wa Daraja la Matetema (Wilaya ya Kaskazini "B" Unguja):** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wakala wa Barabara ulipanga kulijenga daraja la Matetema pamoja na barabara zinazoingia kwenye daraja (road approach) zenye urefu wa mita 40 kila upande

kwa kiwango cha kifusi. Kazi za Ujenzi zinafanywa na Kampuni ya OCRA kutoka Dar es Salaam ikisimamiwa na Wakala wa Barabara Zanzibar. Ujenzi huu utachukuwa muda wa miezi sita (6) na hadi kufikia Machi 2024, kazi iliyofanyika ni kusaini Mkataba wa ujenzi na Mkandarasi na kazi za ujenzi zinatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi wa Mei, 2024. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, jumla ya **TSH 540,000,000** zilitengwa na hadi kufikia Machi 2024, jumla ya **TSH 378,000,000** zilipatikana sawa na **asilimia 70** ya makadirio ya mwaka.

l. **Ujenzi wa Daraja la Machui (Wilaya ya Kati - Unguja):** Wakala imepanga kujenga daraja la Machui na barabara zinazoingia kwenye daraja hilo (road approach) urefu wa mita 40 kila upande kwa kiwango cha kifusi. Kazi za ujenzi zitatekelezwa na Mkandarasi Kampuni ya OCRA kutoka Dar es Salaam ikisimamiwa na Wakala wa Barabara na muda wa utekelezaji ni miezi sita (6). Hadi kufikia Machi 2024, Mkataba wa ujenzi umeshasainiwa baina ya Wakala wa Barabara na Mkandarasi na kazi za ujenzi zimepangwa kuanza mwishoni mwa mwezi wa Mei, 2024. Kwa mwaka wa fedha, 2023/2024 ujenzi huu umepangiwa kutumia jumla ya **TSH 670,000,000**, na hadi kufikia Machi 2024, jumla ya **TSH 268,000,000** zimepatikana sawa na **asilimia 40** ya makadirio ya mwaka.

m. **Uimarishaji wa Usalama Barabarani kwa Unguja na Pemba**: Wakala wa Barabara Zanzibar inaendelea na kazi ya uwekaji wa alama mbalimbali na michoro ya usalama barabarani katika maeneo tofauti. Barabara zilizopangwa kuwekewa michoro na alama za barabarani Unguja na Pemba zina jumla ya urefu wa kilomita 48. Barabara hizo ni Ole-Kengeja (35km), Mchangamle - Residence Zanzibar (4.5km) na Mwanakwerekwe Makaburini - Kituo cha Polisi Fuoni (8.6km). Hadi kufikia Machi 2024, Wakala wa Barabara umekamilisha kazi ya tathimini ya kumpata Mkandarasi na inaanda rasimu ya mkataba kwa ajili ya kukamilisha taratibu za kumpata Mkandarasi. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, jumla ya **TSH 748,000,000** zilitengwa kwa ajili ya kazi hiyo na zimepatikana zote.

n. **Matengenezo ya Kawaida ya Barabara:** Wakala wa Barabara ilipanga kuzifanyia matengenezo ya kawaida barabara za Unguja na Pemba zenye jumla ya urefu wa kilomita 541 (Unguja 362km na Pemba 179km). Kazi zilizopangwa kufanyika ni ukataji wa majani pembezoni mwa barabara, kung'oa visiki, kusafisha misingi ya maji ya mvua, makalvati na madaraja pamoja na uzibaji wa mashimo kwenye barabara zilizojengwa kwa lami ambapo jumla ya mita za mraba 8,200 zilipangwa kuzibwa kwa Unguja na Pemba. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya kilomita 547.5 (Unguja 368.5km na 179km Pemba) zimefanyiwa usafi wa ukataji wa majani pembezoni mwa barabara, usafishaji wa misingi ya maji na makalvati/madaraja sawa na asilimia 101 ya makadirio. Kwa upande wa uzibaji wa mashimo katika barabara, jumla ya mita za mraba 6,109 zilifanyiwa matengenezo kwa kuzibwa mashimo (Unguja mita za mraba 4,789 na Pemba mita za mraba1,320) sawa na **asilimia 122.18** za makadirio. Kiambatanisho Nambari 3A na 3B kinahusika. Kwa mwaka wa fedha, 2023/2024, jumla ya TSH 1,097,658,845 zilipangwa kutumika kwa ajili ya matengenezo ya kawaida ya Barabara na hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya **TSH 972,706,295** zimepatikana sawa na asilimia 88.6 ya makadirio ya mwaka.

o. **Uendeshaji wa Shughuli za Ofisi:** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wakala wa Barabara ilipanga kuendelea kuimarisha mazingira ya kazi kwa watumishi pamoja na kuwajengea uwezo wafanyakazi 49 kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu. Hadi kufikia Machi, 2023 Wakala imefanikiwa kununua vifaa mbali mbali vya ofisi, kusimamia maslahi ya watumishi pamoja na kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi 38 na mafunzo ya muda mrefu mfanyakazi mmoja (1) sawa na **asilimia 79.6** ya makadirio ya mwaka.

21. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wakala wa Barabara Zanzibar ilipangiwa kutumia jumla ya **TSH 5,216,470,000** ikiwa ni ruzuku kwa kazi za kawaida na Mshahara, na **TSH 3,961,673,918** zilipangwa kwa kipindi cha Julai – Machi, 2024. Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya **TSH 3,685,297,202.39** zimetumika sawa na **asilimia 93** ya

makadirio ya miezi tisa na **asilimia 70.6** makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, **TSH 3,536,565,015** ni Mshahara na **TSH 148,732,187.39** ni matumizi ya kawaida.

22. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wakala wa Barabara ilipangiwa kutumia jumla ya **TSH 12,701,754,845** kwa ajili ya matengenezo ya Barabara Unguja na Pemba. Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **TSH 8,072,146,295** zimepatikana (Unguja **TSH 4,819,646,295** na Pemba **TSH 3,252,500,000**) sawa na **asilimia 63.5** ya makadirio ya bajeti. Fedha hizi zilitengwa kupitia bajeti ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar.

## IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

23. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia Programu ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji ina jukumu la kuratibu na kusimamia miradi mbalimbali ya maendeleo katika sekta ya Ujenzi, Usafirishaji na Mawasiliano inayotekelezwa na Wizara. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia programu ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji ilipanga kusimamia na kuratibu utekelezaji wa miradi ifuatayo:-

## MIRADI YA UIMARISHAJI WA MIUNDOMBINU YA USAFIRI WA BARABARA

a. **Barabara za Mjini Unguja Zenye Urefu wa Kilomita 100.9:** Wizara inaendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Barabara za Mjini zenye urefu wa kilomita 100.9 pamoja na ujenzi wa barabara za juu (Fly over) katika eneo la Amani na Mwanakwerekwe Round About. Mradi huu unahusisha ujenzi na utanuzi wa Barabara, ujenzi wa njia za wetembea kwa miguu, taa za barabarani, taa za kuongozea magari (Trafic light), michoro ya kugawa barabara (road marking) na alama za barabarani za kuonyesha mipindo, kasi ya mwendo unaotakiwa na alama za wanaokatisha barabara, pia ujenzi wa barabara hizi umezingatia watu wenye uhitaji maalum. Ujenzi wa barabara hizi unatekelezwa na Kampuni ya CCECC kutoka nchini China na Msimamizi

wa ujenzi ni Kampuni ya Dar-al-handasa kutoka Lebanon. Mkataba wa Ujenzi ulisainiwa tarehe 6 Agosti, 2022 kwa gharama ya fedha za Kimarekani **USD 116,131,442.96** na kuanza rasmi tarehe 1 Disemba, 2022 na unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 36. Fedha za mradi huu zinatolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 jumla ya kilomita 70.25 kati ya 100.9km sawa na **asilimia 69.62** zinaendelea kujengwa na zipo katika hatua mbali mbali na jumla kilomita 35 tayari zimeshawekwa lami na zege. Kwa upande wa ujenzi wa barabara za juu (Flyover) katika eneo la Mwanakwerekwe umeanza na umefikia asilimia 21.54 ya utekelezaji. Mradi huu kwa ujumla hadi kufikia Machi 2024 umefikia asilima 34 ya utekelezaji. **Kiambatanisho Nambari 4 kinahusika.**

Kwa mwaka wa fedha, 2023/2024, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya **TSH 80,100,000,000** kutoka Serikalini na hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **TSH 63,813,146,617** zimepatikana sawa na **asilimia 80** ikiwa ni malipo ya Mkandarasi, Mshauri Elekezi na malipo ya fidia kwa wananchi walioathirika na mradi huu.

b. **Barabara za Ndani Zenye Urefu wa Kilomita 275.9 Unguja na Pemba:** Wizara inaendelea na ujenzi wa barabara za ndani zenye urefu wa kilomita 275.9. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kazi za ujenzi zinatekelezwa na Kampuni ya IRIS/ASER kutoka Nchini Uturuki ambayo ilisaini Mkataba wa Ujenzi tarehe 22 Novemba, 2021 kwa gharama za **USD Milioni 80.3** ikiwa ni gharama za ujenzi. Mradi huu ulianza rasmi tarehe 26 Machi, 2022 na unatarajiwa kukamilika mwezi wa Julai, 2025. Ujenzi wa barabara hizi unasimamiwa na Wakala wa Barabara Zanzibar. Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, jumla ya kilomita 10 zimekamilika kwa kiwango cha lami na jumla ya kilomita 49.6 zimekamilika kwa kiwango cha kifusi kwa Unguja, kwa upande wa Pemba, jumla ya kilomita 13.8 zimekamilika kwa kiwango cha kifusi. Kwa ujumla kazi za ujenzi zinaendelea kwa barabara mbalimbali katika hatua tofauti Unguja na Pemba. Mradi huu hadi kufikia mwishoni mwa mwezi wa Machi, 2024 umefikia **asilimia 41** ya utekelezaji. **Kiambatanisho Nambari 5 kinahusika.**

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya **TSH 44,060,000,000**. Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya **TSH 16,457,281,262.19** zimepatikana sawa na **asilimia 37** ya makadirio ya bajeti.

c. **Barabara Kuu za Zanzibar:** Mradi huu unajumuisha ujenzi wa barabara kuu za Unguja na Pemba zikiwemo Tunguu – Makunduchi kilomita 48, Fumba – Kisauni kilomita 12, Mkoani - Chake Chake kilomita 43.5 pamoja na barabara ya Chake – Wete kilomita 22.1. Utekelezaji wa mradi huu hadi kufikia mwishoni mwa mwezi wa Machi, 2024 ni kama ifuatavyo:-

   i. **Barabara ya Tunguu - Makunduchi, Fumba – Kisauni na Barabara ya Mkoani – Chake:** Barabara hizi zitajengwa na Mkandarasi Kampuni ya PROPAV/MECCO JV kwa mkopo kutoka "United Kingdom Export Finance – UKEF", kwa gharama ya Euro 230,798,792.41 ambapo Wizara imeshasaini Mkataba wa Ujenzi tokea mwezi wa Septemba, 2022. Hadi kufikia Mwezi Machi, 2024, mkandarasi anaendelea na hatua za kukamilisha kazi za usanifu na michoro pamoja na kazi za mapitio ya tathmini za fidia (Ressetlement Action Plan - RAP) kwa barabara hizo.

   ii. **Barabara ya Chake - Wete 22.1km:** Wizara inaendelea na ujenzi wa barabara ya Chake-Wete ambapo kazi za ujenzi wa barabara hiyo inayotekelezwa na Kampuni ya Mwananchi Engineering Company Limited (MECCO) kutoka Dar -es – Salaam chini ya usimamizi wa Mshauri Elekezi Kampuni ya Dar al Handasah kwa ufadhili wa BADEA, SAUDI FUND na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Muda wa utekelezaji wa mradi huu ni miezi 30 na ulianza rasmi mwezi wa Februari 2022 na unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba 2024. Mradi huu unatarajiwa kutumia TSH Bilioni 23.6 kwa ajili ya ujenzi na USD 1,076,100 kwa ajili ya kazi za usimamizi wa mradi.

   Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 jumla ya kilomita 14.5 zimejengwa katika matabaka tafauti ya kifusi pamoja na uwekaji lami nyepesi (Primer) kwa eneo la kilomita 0.7 sambamba na ujenzi wa

Madaraja makubwa matatu (3) likiwemo Daraja la Piki, Machengwe pamoja na Weni. Aidha, Wizara kwa hatua za awali imekamilisha ulipaji wa fidia za nyumba zitakazoathirika kutokana na ujenzi wa barabara hiyo kutoka Melitano hadi Limbani. Kwa eneo la Wete Mjini, Wizara inasubiri ripoti ya tathmini kutoka kwa Mthamini Mkuu wa Serikali ili iweze kufanya malipo. Mradi huu umefikia asilimia 25 ya utekelezaji.

iii. **Ujenzi wa barabra ya Jozani – Charawe – Ukongoroni (23.3km), Fuoni – Tunguu (5.8km), barabara ya Bungi (0.9km) na Barabara ya Uwanja wa Ndege wa Nungwi (2.5km):** Wizara ilipanga kuzijenga barabra ya Jozani – Charawe – Ukongoroni (23.3km), Fuoni – Tunguu (5.8 km), barabara ya Bungi ( 0.9km ) na Barabara ya Uwanja wa Ndege wa Nungwi (2.5km) kwa kiwango cha lami. Kazi za ujenzi wa barabara hizi zinatekelezwa na Kampuni ya ORKUN. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, Wizara imefanikiwa kukamilisha kilomita 19.3 za barabara ya Jozani – Charawe – Ukongoroni (23.3km) kwa kiwango cha lami. Pia, Wizara imekamilisha ujenzi wa Barabara ya Fuoni – Tunguu yenye urefu wa kilomita 5.8, barabara ya Bungi yenye urefu wa kilomita 0.9 na barabara ya Uwanja wa Ndege wa Nungwi yenye urefu wa kilomita 2.5.

24. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Ujenzi wa Barabara kuu ulipangiwa kutumia jumla ya **TSH 249,387,000,000.** Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya **TSH 145,270,914,793.69** zimepatikana sawa na asilimia 58 ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo, **TSH 1,737,020,090.00** zinatoka kwa BADEA na SAUDI FUND, **TSH 87,685,077,208.6** zinatoka kwa UKEF na **TSH 55,848,817,495** ni kutoka Serikalini.

**MIRADI YA UIMARISHAJI WA MIUNDOMBINU YA USAFIRI WA ANGA**

d. **Uwanja wa Ndege wa Pemba:** Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ina lengo la kuimarisha Uwanja wa Ndege wa Pemba kwa kuongeza urefu wa barabara ya kutua na kurukia ndege (runway and taxi way), kujenga jengo jipya la abiria

(Terminal Building) na miundombinu husika itakayowezesha uwanja huo kutua ndege aina ya Code C (Boeing 737-800) na zinazolingana. Aidha, Mkataba wa ujenzi wa Uwanja huo baina ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi na Kampuni ya PROPAV/MECCO JV umeshasainiwa tokea mwezi Januari, 2023. Hadi kufikia mwezi Machi, 2024, kazi iliyofanyika ni malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha eneo la ujenzi wa mradi (Project Construction area) ambapo jumla ya **TSH 12,627,519,000** ziliingizwa kutoka Serikalini kwa kuwalipa wananchi 818 ambapo hadi sasa wananchi 744 wameshalipwa na zoezi la malipo bado linaendelea.

25. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya **TSH 160,000,000,000**. Kati ya fedha hizo **TSH 10,000,000,000** ni kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na **TSH 150,000,000,000** ni kutoka kwa Mfadhili. Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **TSH 90,782,337,450** zimepatikana sawa na **asilimia 56.7** ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, **TSH 30,543,129,000** ni kutoka Serikalini na **TSH 60,239,208,450** ni kutoka kwa Mfadhili (UKEF) ikiwa ni malipo ya awali (Advance Payment) kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi. Ongezeko la fedha kutoka Serikalini linatokana na mahitaji ya malipo ya mradi wa Ujenzi wa Terminal II katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume ambapo jumla ya **TSH 17,805,000,000** zilitumika kumlipa Mkandarasi.

**MIRADI YA UIMARISHAJI WA MIUNDOMBINU YA USAFIRI WA BAHARINI**

**e. Bandari Jumuishi ya Mangapwani**

i. **Ujenzi wa Bandari ya Mangapwani: Wizara imepanga kujenga Bandari Jumuishi ya Mangapwani.** Kwa kuzingatia mahitaji ya kukamilisha ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mwangapwani, Wizara imeingia mkataba na Kampuni ya CHEC kwa mkataba wa Usanifu, ujenzi na utafutaji fedha (EPC+F). Makubaliano hayo yamefikiwa baada ya Serikali kujiridhisha na Upembuzi yakinifu ambao unaendana na Mpango Mkuu wa Bandari (Integrated Port Masterplan). Hivi sasa

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea na hatua za kukamilisha upatikanaji wa fedha za Ujenzi wa Bandari hiyo EXIM BANK ya China na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

ii. **Ujenzi wa Miundombinu ya Barabara katika Eneo la Mangapwani:** Wizara inaendelea na ujenzi wa Barabara za ndani (ring road) katika eneo la mradi wa Bandari Jumuishi ya Mangapawani zenye urefu wa kilomita 12 kama zilivyoainishwa ndani ya Mpango Mkuu wa Bandari hiyo. Kazi za ujenzi wa barabara hizo zinatekelezwa na Kampuni ya ORKUN ambayo imepewa mkataba wa miezi kumi na nane (18) kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo zenye gharama za dola za kimarekani USD 35,572,500. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi 2024, jumla ya kilomita 5.8 zimesafishwa na kuwekea tabaka mbali mbali za kifusi. Kati ya hizo kilomita 4.35 tayari zimeshawekwa lami ya mwanzo ya maji (Prime coat). Jumla ya **USD 12,000,000** wastani wa **asilimia 33.7** zimeshalipwa katika ujenzi huo. Aidha, Wizara imekamilisha kulipa fidia kwa kilomita 5.8 na inaendelea na hatua za ulipaji wa fidia kwa kilomita 6.2 ili kutoa nafasi ujenzi huo uendelee. Mradi huu umefikia kiasi cha **asilimia 35** ya utekelezaji.

iii. **Ujenzi wa Nyumba za Fidia katika eneo la Mangapwani na Bumbwini:** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeingia mkataba na Kampuni ya ORKUN kwa ajili ya Ujenzi wa nyumba 370 za fidia ambazo zitajengwa katika eneo la Bumbwini na Mangapwani kwa muda wa miezi 18. Mradi huo utagharimu jumla ya **USD 23,994,750** na hadi kufikia Machi 2024, Jumla ya **USD 4,000,000** zimetumika sawa na **asilimia 16.67.** Kwa sasa ujenzi wa nyumba 110 unaendelea katika hatua mbali mbali ikiwemo ujenzi wa misingi, kuta na paa. Mradi huu umefikia kiasi cha **asilimia 20**. Aidha, Wizara imekamilisha malipo ya fidia katika eneo la Kidanzini kwa Mbara, Bumbwini lenye hekta 40.

Kwa mwaka wa fedha, 2023/2024, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya **TSH 20,000,000,000** kutoka Serikalini na hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya **TSH 28,469,655,304** zimepatikana sawa na asilimia 142 ya makadirio ya bajeti. Fedha hizi za ziada zimehaulishwa kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya fedha kwenye mradi huu.

26. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia Programu ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji ilipangiwa kutumia jumla ya **TSH 553,547,000,000** kwa kazi za maendeleo. Kati ya fedha hizo, **TSH 324,000,000,000** ni mkopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na **TSH 229,547,000,000** ni mchango kutoka Serikalini.

Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **TSH 344,793,335,427.15** zimetumika sawa na **asilimia 62** ya makadirio. Kati ya fedha hizo, **TSH 149,661,305,748.60** ni mkopo kutoka kwa Washirika wa maendeleo sawa na **asilimia 46.2** ya makadirio na **TSH 195,132,029,678.5** ni mchango wa Serikali sawa na **asilimia 85** ya makadirio ya bajeti.

## C.3. 2. PROGRAMU YA UJENZI NA MAJENGO YA SERIKALI

27. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ina lengo la kuhakikisha kuwepo kwa usimamizi imara katika kazi za ujenzi na majengo bora ya Serikali na binafsi yaliyo salama na yenye viwango vinavyokubalika kwa mujibu wa miongozo iliyopo na yenye kukidhi mahitaji ya watumiaji wote. Matokeo yanayotarajiwa ni kuwepo kwa ujenzi uliosalama pamoja na majengo bora yenye kukidhi mahitaji ya watumiaji wote. Programu hii ina programu ndogo moja (1) ambayo ni Programu ya Usimamizi wa Ujenzi na Majengo ya Serikali.

### C.3.2.1. Programu ndogo ya Usimamizi wa Ujenzi na Majengo ya Serikali.

28. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Wakala wa Majengo, Bodi ya Usajili wa Wakandarasi na Bodi ya Usajili wa Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo. Programu hii ina lengo la kuhakikisha kuwepo kwa usimamizi imara wa ujenzi na majengo bora ya Serikali na binafsi yaliyosalama na yenye viwango vinavyokubalika kwa mujibu wa miongozo iliyopo. Kupitia programu hii ndogo Wizara imeweza kutekeleza yafuatayo:-

## WAKALA WA MAJENGO ZANZIBAR

29. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Majengo ina jukumu la kuendeleza majengo ya Serikali, kujenga, kukodisha (Lease or Rent) na kukopesha Majengo ya Serikali kwa bei nafuu kwa watumishi wa umma wanaostahiki, kuandaa na kuweka utaratibu mzuri wa kudhibiti makaazi ya watumishi wa umma, kutoa huduma za Ushauri wa Ujenzi, kusimamia Majengo ya Serikali pamoja na kupanga ujenzi wa Majengo ya Serikali kulingana na mahitaji.

30. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, Wakala wa Majengo Zanzibar imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

    a. **Kuandaa Nyaraka za Ujenzi.** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wakala wa Majengo ilipanga kuandaa nyaraka za ujenzi 29 na hadi kufikia Machi, 2024, imefanikiwa kuandaa nyaraka 20 za ujenzi (Ramani na Gharama) sawa na **asilimia 69** ya makadirio ya mwaka. Kati ya nyaraka hizo, 9 zimeandaliwa Unguja na 11 zimeandaliwa Pemba. **Kiambatanisho nambari 6A** kinaonesha mchanganuo wa nyaraka za ujenzi zilizoandaliwa.

    b. **Usimamizi wa Miradi ya Ujenzi.** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wakala wa Majengo ilipanga kusimamia miradi ya ujenzi 30 na hadi Machi, 2024, imefanikiwa kusimamia miradi ya ujenzi 42 (Construction Supervision) sawa na **asilimia 140**. Kati ya miradi hiyo 25 imesimamiwa Unguja na 17 imesimamiwa Pemba. **Kiambatanisho nambari 6B kinaonesha kazi zilizosimamiwa.**

    c. **Kuandaa Rasimu ya Sheria ya Wakala wa Majengo.** Wakala wa Majengo kwa kushirikiana na Wizara imefanikiwa kuandaa rasimu ya sheria ya Wakala wa Majengo ambayo itaiwezesha taasisi hiyo kufanya kazi zake kwa ufanisi. Rasimu hiyo ipo katika hatua ya kuwasilishwa kwa Wadau mbalimbali ili kupatiwa maoni.

**Mapato na Matumizi**

31. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai – Machi, 2024, Wakala ilipanga kukusanya jumla ya **TSH 273,500,000** kutoka katika vianzio vyake na hadi kufikia Machi, 2024, imefanikiwa kukusanya jumla ya **TSH 153,988,357** sawa na **asilimia 56.3** ya makadirio ya kipindi cha miezi tisa (9). Kati ya fedha hizo, **TSH 152,368,357**. zimekusanywa Unguja na **TSH 1,620,000** zimekusanywa Pemba.

    Kwa upande wa matumizi, Kwa mwaka 2023/2024, Wakala wa Majengo ilipangiwa kutumia jumla ya **TSH 473,200,000** na kwa kipindi cha Julai – Machi, 2024, ilipangiwa kutumia jumla ya **TSH 391,200,000** na hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **TSH 101,807,960** zimetumika sawa na **asilimia 26** ya miezi tisa na **asilimia 22** ya mwaka kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

**BODI YA USAJILI WASANIFU, WAHANDISI NA WAKADIRIAJI MAJENGO**

32. **Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Usajili, Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo ina jukumu la kusajili Wasanifu, Wahandisi, Wakadiriaji Majengo, Makampuni ya kiushauri wa kada za Usanifu, Uhandisi, Wakadiriaji Majengo pamoja na kuratibu mikutano na semina zinazohusiana na kada hizo.

33. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo imefanikiwa kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

    a. **Kusajili Wataalamu wa Ujenzi.** Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 , Bodi ya Usajili, Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo ilikadiria kusajili jumla ya wataalamu 74 na hadi kufikia Machi 2024 imefanikiwa kusajili jumla ya wataalamu 76 sawa na asilimia 102.7. Kati ya wataalamu hao, Washauri elekezi wazalendo 20, Mshauri elekezi wa Kigeni 1, Kampuni za ushauri za kizalendo 7 , Kampuni ya Ushauri ya kigeni 1, Wataalamu mahiri wazalendo 11, Wataalamu mahiri wa kigeni 6, Wahitimu 28 pamoja na fundi sadifu 2.

b. **Usajili wa miradi.** Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi 2024, Bodi ilikadiria kusajili miradi 210 na hadi kufikia Machi 2024, Bodi imefanikiwa kusajili miradi 234 sawa na asilimia 111.4 katika maeneo mbali mbali ya ujenzi kwa Unguja na Pemba, miradi hiyo inajumuisha Majengo ya Biashara, Nyumba za Makaazi, Hoteli, Shule, Nyumba za Ibada na mengineyo.

c. **Kufanya ukaguzi katika maeneo ya Ujenzi.** Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi 2024, Bodi imefanikiwa kufanya ukaguzi wa maeneo ya Ujenzi 24 kwa Unguja na Pemba.

d. **Kutoa elimu kwa Wadau mbalimbali wa Ujenzi.** Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 Bodi ya Usajili, Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo imefanikiwa kutoa elimu kwa wadau mbali mbali ikiwemo ofisi za Serikali na sekta binafsi kwa lengo la kuwapa uwelewa juu ya umuhimu wa kuwasajili wataalamu wake ambao wamepewa dhamana za kusimamia majengo kwa mujibu wa sheria. Vilevile Bodi kwa kushirikiana na Taasisi ya Usanifu, Uhandisi na Ukadiriaji ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano imefanya mafunzo mafupi ya kuwaendeleza wahitimu ili kuwajengea uwezo katika kutatua migogoro ya ujenzi kwa kutumia taratibu za kisheria.

e. **Kukuza mashirikiano na Taasisi za nje ya Zanzibar.** Pia Bodi imeingia mkataba wa mashirikiano (MoU) ya kikazi na Bodi za Tanzania (ERB na AQRB) kwa lengo la kubadilishana uzoefu katika kazi pamoja na kufanya mafunzo ya kuwaendeleza wataalamu kwa pamoja.

**Mapato na Matumizi**

34. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Bodi ya Usajili, Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo ilikadiria kukusanya Jumla ya **TSH 527,000,000** na hadi kufikia machi, 2024 jumla ya **TSH 406,395,500** zimekusanywa sawa na **asilimia 77** ya makadirio ya mwaka.

Kwa upande wa matumizi, Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Bodi ya Usajili, Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo ilipangiwa kutumia jumla ya **TSH 342,300,000** na hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya **TSH 108,286,000** zimetumika sawa na **asilimia 31.6** ya makadirio ya bajeti ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini.

**BODI YA USAJILI WA WAKANDARASI.**

35. **Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Usajili wa Wakandarasi ina jukumu la kufanya usajili wa wakandarasi na kutunza Daftari la Wakandarasi, kusimamia shughuli za Wakandarasi, kupanga na kutoa mafunzo, warsha, makongamano juu ya masuala yanayohusiana na ujenzi, kuweka vigezo na madaraja mbalimbali ya Wakandarasi kwa ajili ya usajili pamoja na kupokea, kuchunguza na kusikiliza malalamiko dhidi ya Wakandarasi.

36. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Bodi ya Usajili wa Wakandarasi imefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

a. **Usajili wa Wakandarasi Wapya:** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Bodi ya Usajili wa Wakandarasi ilikadiria kusajili Wakandarasi wapya 56 na hadi kufikia Machi, 2024 imefanikiwa kusajili Wakandarasi wapya 57 sawa na **asiliamia 101** ya makadirio ya mwaka.
b. **Usajili wa Miradi:** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Bodi ilipanga kusajili miradi 220 na hadi kufikia Machi, 2024 imefanikiwa kusajili miradi 148 sawa na **asilimia 67.2** ya makadirio ya mwaka.
c. **Ukaguzi wa Miradi:** Kwa mwaka 2023/2024, Bodi ilipanga kukagua miradi 100 na hadi kufikia Machi, 2024 imefanikiwa kufanya ukaguzi wa miradi 65 sawa na **asilimia 65** ya makadirio ya mwaka. Aidha, Bodi imechukuwa hatua za kisheria na kinidhamu kwa Wakandarasi 29 waliokiuka sheria.

**Mapato na Matumizi**

37. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Bodi ya Usajili wa Wakandarasi ilikadiria kukusanya jumla ya **TSH 1,657,713,000,**

na kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 ilikadiria kukusanya jumla ya **TSH 1,150,510,500**. Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya **TSH 682,604,900** zimekusanywa sawa na **asilimia 59.3** ya makadirio ya miezi tisa na **asilimia 41.1** ya makadirio ya mwaka.

Kwa upande wa matumizi, Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Bodi ya Usajili wa Wakandarasi ilipangiwa kutumia jumla ya **TSH 197,120,000** na kwa kipindi cha miezi tisa ilipangiwa kutumia **TSH 141,056,000** na hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya **TSH 47,098,099** zimetumika sawa na **asilimia 33** ya makdirio ya miezi tisa na **asilimia 24** ya makadiri ya bajeti ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini.

### C.3.3. PROGRAMU YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA)

**38. Mheshimiwa Spika,** programu hii ina lengo la kuhakikisha kuwepo kwa miundombinu na huduma bora za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) Zanzibar. Matokeo yanayotarajiwa ni kuwepo kwa miundombinu na huduma bora za TEHAMA. Programu hii ina programu ndogo moja (1) ambayo ni Programu ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA.

### C.3.3.1. Programu Ndogo ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA.

**39. Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Idara ya Mawasiliano na ina lengo la kuhakikisha kuwepo kwa miundombinu na huduma bora ya TEHAMA zilizo salama na endelevu. Wizara kupitia programu hii ndogo imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

### IDARA YA MAWASILIANO

**40. Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mawasiliano kupitia programu ndogo ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA ina jukumu la kuratibu huduma za mawasiliano ya simu, posta na Anuani za makaazi, mtandao (intaneti) pamoja na kusimamia maendeleo ya huduma za TEHAMA Zanzibar ili kufikia uchumi wa kidijitali.

41. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Idara ya Mawasiliano ilipanga kuratibu huduma za mawasiliano ya simu, intaneti pamoja na huduma za TEHAMA, kuratibu na kusimamia Ujenzi wa Minara katika visiwa vya Unguja na Pemba, mafunzo ya TEHAMA kupitia vituo vya TEHAMA Jamii, kuendeleza matumizi ya mfumo wa Anuani za Makaazi pamoja na kuratibu uanzishaji wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

42. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, Idara ya Mawasiliano imefanikiwa kutekeleza yafauatayo:-

a. **Ujenzi wa Minara ya Mawasiliano:** Jumla ya Minara 18 ilijengwa Zanzibar katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba ambayo yalionekana kuna changamoto ya mawasiliano. Minara 9 imejengwa Unguja na Minara 9 imejengwa Pemba. **Kiambatanisho nambari 7A.** Ujenzi wa Minara hii ni muendelezo wa juhudi za Serikali katika kuhakikisha huduma za Mawasiliano katika maeneo yote ya Zanzibar zinapatikana kwa asilimia mia moja. Ujenzi wa Minara hii inajumuisha idadi ya Minara 474 ya Mawasiliano inayotoa Huduma za sauti na Data hapa Zanzibar. Hali halisi ya upatikanaji wa Huduma ya Mawasiliano hivi sasa inakadiriwa kufikia asilimia 100 katika maeneo yenye makaazi ya Watu. Tathmini iliyofanywa mwezi Septemba 2023 na Wizara ikishirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inaonesha kuwa huduma za Mawasiliano zinapatikana kwa angalau mtandao mmoja wa mtoa Huduma za simu katika Shehia zote 388 za Zanzibar.

   Upatikanaji wa Huduma za Mawasiliano umeimarika zaidi kwa kuwepo Teknolojia ya 5G katika maeneo ya mjini Unguja, Kaskazini Unguja, Kusini Unguja na Chake Chake Pemba, ambapo minara 50 katika maeneo hayo inatoa mawasiliano ya 5G. Aidha, Hali ya upatikanaji wa Mawasiliano ya sauti na data kwa upande wa Zanzibar ni zaidi ya lengo la asilimia themanini (80%) iliyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 katika Ibara ya 61(f) inayotaka "kuongeza wigo na matumizi ya mawasiliano ya kasi (broadband services) kutoka **asilimia 45** mwaka 2020 hadi asilimia 80 kwa mwaka 2025".

b. **Ukaguzi wa Upatikanaji wa Huduma za Mawasiliano:** Idara ya Mawasiliano kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inaendelea na ukaguzi na uchambuzi wa upatikanaji wa Huduma za Mawasiliano katika maeneo ya visiwa vidogo vidogo 48 hapa Zanzibar. Visiwa hivyo pia vimetambuliwa kama maeneo muhimu yanayohitaji ufuatiliaji wa karibu wa huduma za mawasiliano ili kuendana na Sera ya Uchumi wa Buluu, kuongeza ulinzi wa nchi na kuwezesha shughuli za kitalii kwenye visiwa vinavyotumika kwa utalii. Hali ya upatikanaji wa mawasiliano katika visiwa vidogo imeanishwa katika Kiambatanisho namba 7B ambapo kati ya visiwa arobaini na nane (48) vilivyotathminiwa, ni visiwa kumi na moja tu (11) vinavyohitaji maboresho.

c. **Utoaji Mafunzo ya TEHAMA kupitia Vituo vya TEHAMA Jamii**: Wizara kupitia Idara ya Mawasiliano kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi, 2024 ilipanga kutoa mafunzo na huduma za TEHAMA kwa wananchi 1875 na imefanikiwa kutoa mafunzo na huduma za TEHAMA kwa wanajamii wapato 1186 sawa na asilimia 63. Kati ya wananchi waliohudumiwa, wanawake ni 724 na wanaume ni 462 kupitia vituo vya TEHAMA Jamii kutoka katika wilaya zote 11. Lengo la mafunzo haya ni kupunguza idadi ya wanajamii wasiojua kutumia kompyuta na mitandao ili waweze kushiriki katika uchumi wa kidijitali.

d. **Kuendeleza Matumizi ya Mfumo wa Anuani za Makaazi:** Wizara inaendelea kusimamia na kuratibu matumizi ya Anuani za Makaazi ambapo katika kuhakikisha mfumo wa Anuani za Makaazi unaimarika na kutumika ili kuleta manufaa kwa Jamii, tayari baadhi ya mifumo ya utoaji huduma imeunganishwa na mfumo wa Anuani za Makazi wa NaPA ili kurahisisha utoaji wa huduma za kidijitali kwa mfano utoaji wa huduma ya kubaini mahala ulipo "location". Huduma hii inasaidia kubaini jengo au mtu mahala halisi alipo kwa kutumia mifumo ya kidijitali, pia inasaidia vyombo vya uokozi pamoja na vyombo vya ulinzi kubaini kwa haraka mahali husuka.

e. **Kuratibu Uanzishaji wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi:** Wizara kupitia Idara ya Mawasiliano iliratibu uanzishaji wa Tume ya

Ulinzi wa Taarifa Binafsi chini ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya Mwaka 2022. Tume hii ilianza kazi tarehe 1 mei 2023 ambayo lengo lake kuu ni kulinda taarifa binafsi na kuimarisha ulinzi wa taarifa pamoja na kulinda faragha za watu kwa mujibu wa sheria. Tume hii inafanya kazi Tanzania bara na Zanzibar kwenye taasisi zote za Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

43. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu hii ndogo ya Usimamizi wa Huduma za Mawasiliano na TEHAMA ilipangiwa kutumia jumla ya **TSH 6,599,771,000** kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo. Kati ya fedha hizo, **TSH 400,700,000** ni matumizi mengineyo, **TSH 299,071,000** ni mshahara na **TSH 5,900,000,000** ni kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **TSH 1,719,175,594.2** zimetumika sawa na **asilimia 26** ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo, **TSH 213,386,907** ni mshahara, **TSH 85,380,000** ni matumizi mengineyo na **TSH 1,420,408,687.25** ni kwa ajili ya kazi za maendeleo.

## C.3.4. UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI

44. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ina lengo la kuhakikisha kuwa Wizara inaratibu na kutayarisha Sera na Mipango bora katika Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji pamoja na usimamizi mzuri wa rasilimali watu. Programu hii ina programu ndogo tatu (3) ambazo ni:- Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji, Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara pamoja na Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba.

### *C.3.4.1. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji*

45. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi na ina lengo la kuimarisha huduma za ofisi na usimamizi wa rasilimali watu.

## IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

**Mheshimiwa Spika,** Idara hii imepewa jukumu la kusimamia na kutathmini shughuli za uendeshaji wa Wizara na kushughulikia maslahi pamoja na nidhamu kwa wafanyakazi. Aidha, Idara inaandaa na kusimamia mpango wa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa wafanyakazi wa Wizara pamoja na utunzaji wa kumbukumbu na mali za Wizara. Pia, Idara inajukumu la kuimarisha mazingira mazuri ya utendaji kazi kwa kuhakikisha vitendea kazi vinapatikana kwa wakati. Vilevile, Idara inatoa huduma za ununuzi na usimamizi wa mapato na matumizi ya Wizara.

46. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Idara ya Uendeshaji na Utumishi kupitia programu ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji ilipanga kuwajengea uwezo wafanyakazi 56 wa Wizara kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ili waweze kutoa huduma bora na kwa ufanisi. Aidha, Idara ilipanga kuimarisha huduma za kiutawala na utumishi ikiwemo kuweka mazingira mazuri ya kazi, kusimamia maslahi ya watumishi pamoja na kuongeza vitendea kazi kwa lengo la kuleta ufanisi.

47. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imefanikiwa kuwapatia mafunzo mbalimbali wafanyakazi 49 Unguja na Pemba sawa na **asilimia 87.5** ya wafanyakazi waliopangwa kupatiwa mafunzo hayo. Kati ya hao, wafanyakazi 13 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi tofauti katika Vyuo vya ndani na Nje ya nchi na wafanyakazi 36 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika kozi tofauti. Kiambatanisho Nambari 8A na 8B kinahusika.

48. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha mazingira mazuri ya kazi kwa watendaji yanaimarika, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imezifanyia matengenezo Ofisi, kujenga jengo moja kwa ajili ya Ofisi ya viongozi wa Wizara, kuimarisha vitendea kazi kwa kununua vifaa mbalimbali vya Ofisi pamoja na kuwapatia wafanyakazi stahiki zao ikiwemo malipo ya mishahara, malipo ya likizo pamoja na malipo baada ya saa za kazi.

**49. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Idara ya Uendeshaji na Utumishi kupitia programu ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji ilipangiwa kutumia jumla ya **TSH 2,760,140,000** kwa kazi za kawaida, ikiwa **TSH 1,610,140,000** ni mshahara na **TSH 1,150,000,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **TSH 2,778,415,771** zimetumika sawa na asilimia 100.6 ya makadirio ya Bajeti. Kati ya fedha hizo, **TSH 2,048,616,271** ni Mshahara na **TSH 729,799,500** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

### C.3.4.2. Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara

**50. Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na ina lengo la kuhakikisha Mipango na Sera za Wizara zinatekelezwa.

### IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

**51. Mheshimiwa Spika,** Idara hii imepewa jukumu la kupanga, kuratibu, kusimamia na kutathmini utekelezaji wa Sera na Mipango ya sekta za Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Aidha, Idara inaratibu kazi zote za maendeleo ya Wizara ikiwemo kubuni, kutayarisha na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Pia, Idara inajukumu la kubuni na kufanya tafiti za kisekta ikiwemo ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu.

**52. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara ilipanga kuendelea kuratibu na kufanya tafiti za Wizara, kuendelea kuzifanyia mapitio Sera ya Usafiri ya mwaka 2008 na Sera ya TEHAMA ya mwaka 2013 ili ziendane na mahitaji ya sasa. Vilevile, Idara ilipanga kuratibu na kusimamia miradi ya maendeleo pamoja na kukusanya takwimu mbalimbali katika sekta zinazosimamiwa.

**53. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imefanikiwa kuendelea kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kukusanya takwimu zinazohusu

Wizara, kutayarisha ripoti mbalimbali za utekelezaji wa kazi za Wizara. Aidha, Idara inaendelea kufanya utafiti kuhusiana na uimarishaji wa mfumo wa Usafiri Zanzibar. Matokeo ya utafiti huu yatawezesha Wizara kuwa na Sera bora ya Usafiri pamoja na Mpango Mkuu mpya wa Usafiri Zanzibar utakaopelekea kuwa na huduma za Usafiri zitakazokidhi mahitaji ya wananchi wote ikiwemo wenye mahitaji maalum.

54. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2013, Wizara imekamilisha kuifanyia mapitio Sera hiyo na kwa sasa imeanza matayarisho ya Sera mpya ya kidigital ambayo itahusisha masuala ya TEHAMA. Pia, Wizara imefanikiwa kutayarisha Mpango Mkakati Mpya wa Wizara wa miaka mitatu utakaoanza kutumika kuanzia mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na kuratibu shughuli mbalimbali zinazohusu Sekta ya Ujenzi, Usafirishaji na Mawasiliano na ikiwemo kusimamia na kuratibu Mkutano wa Umoja wa Afrika (AU) wa Mawaziri wa Miundombinu na Nishati uliofanyika Zanzibar mwezi wa Septemba, 2023.

55. **Mheshimiwa Spika,** Idara inaendelea kuratibu Taasisi na Mashirika mbalimbali yanayojitegemea yaliyo chini ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi pamoja na kuratibu na kuandaa vikao vitatu vya ushirikiano baina ya Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Uchukuzi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar vinavyohusu Sekta ya Usafirishaji na Ujenzi kwa lengo kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta hizi. Vikao hivi vimepelekea taasisi zetu kuwa na Hati za Makubaliano (MoU) zitakazowezesha taasisi zetu kushirikiana katika masuala mbalimbali ya kiutendaji na kimafunzo.

56. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kutayarisha Sheria mbalimbali za sekta ya Ujenzi, Usafiri na Mawasiliano ikiwemo Sheria ya uanzishwaji wa Wakala wa Majengo, Sheria ya Karakana, Sheria ya Wakala wa Barabara pamoja na Marekebisho Sheria Namba 5 ya Usafiri wa Baharini ya Mwaka 2006 (Maritime Transport Act no.5 of 2006). Sheria zote hizi ziko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

57. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na

Tafiti za Wizara ilipangiwa kutumia jumla ya **TSH 922,308,000** kwa kazi za kawaida, ikiwa **TSH 342,308,000** ni mshahara na **TSH 580,000,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **TSH 522,285,588** zimetumika sawa na **asilimia 57** ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo, **TSH 240,101,988** ni mshahara na **TSH 282,183,600** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

### C.3.4.3. Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba

**58.** **Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Ofisi Kuu – Pemba na ina lengo la kuhakikisha majukumu ya Wizara kwa upende wa Pemba yanatekelezwa.

### OFISI KUU – PEMBA

**59.** **Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu – Pemba imepewa jukumu la kuratibu na kusimamia kazi zote za Wizara kwa upande wa Pemba. Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, Ofisi Kuu Pemba imeratibu na kusimamia maslahi ya wafanyakazi ikiwemo malipo ya likizo, malipo baada ya saa za kazi, malipo ya safari kikazi pamoja na kufanya malipo ya huduma mbali mbali za uendeshaji. Pia, Ofisi imefanikiwa kuimarisha mazingira ya kazi kwa Wafanyakazi kwa kununua vifaa vya kuendeshea Ofisi pamoja na kufanya matengenezo madogo madogo ya Ofisi. Aidha, Ofisi Kuu imefanikiwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi 2 na muda mfupi wafanyakazi 8 katika fani mbalimbali. Kwa ujumla Ofisi Kuu Pemba imeratibu kwa ufanisi kazi zote zinazofanywa na Wizara kwa upande wa Pemba ikiwemo utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi wa Barabara, Bandari na Viwanja vya Ndege.

**60.** **Mheshimiwa Spika** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Ofisi Kuu Pemba kupitia programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba ilipangiwa kutumia jumla ya **TSH 999,781,000** kwa kazi za kawaida, ikiwa **TSH 499,781,000** ni mshahara na **TSH 500,000,000** ni kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **TSH 656,950,920** zimetumika kwa kazi za kawaida sawa na **asilimia 65.7** ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo, **TSH 505,950,920** ni mshahara na **TSH 151,000,000 ni matumizi men**gineyo.

## D. UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA KWA KIPINDI CHA JULAI, 2023 HADI MACHI, 2024 PAMOJA NA MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

61. **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa bajeti kwa Taasisi zinazojitegemea kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 na malengo yanayotarajiwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ni kama ifuatavyo:-

### D.1. MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI ZANZIBAR

62. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani ina jukumu la kusimamia usafiri barabarani kwa kudhibiti usalama wa watumiaji wa barabara, utoaji wa huduma za usafiri barabarani pamoja na kusimamia Kamati ya Kitaifa ya Usalama Barabarani. Aidha, katika kutekeleza majukumu hayo kwa mujibu wa sheria nambari 7 ya mwaka 2003, Sheria ya Usafiri Barabarani, Mamlaka inafanya shughuli za ukaguzi wa vyombo vya moto na kutoa leseni za njia kwa vyombo hivyo (Road license), kutoa leseni kwa vyuo vya udereva na walimu wao, kutoa leseni za madereva wanafunzi (learner), kuwafanyia majaribio ya nadharia na vitendo madereva wanafunzi, kutoa ruhusa za njia na usafirishaji wa abiria na mizigo, kutoa leseni za vyombo vya biashara, kutoa beji za utingo na madereva pamoja na kutoa vibali na kubadilisha leseni kwa madereva wa kigeni wanaotaka kuendesha vyombo vya moto hapa Zanzibar.

63. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani imetekeleza kazi zifuatazo:-

   a. **Ukaguzi wa Vyombo vya Moto:** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ilipanga kufanya ukaguzi wa vyombo vya moto 67,544 Unguja na Pemba na kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 ilipanga kufanya ukaguzi wa vyombo vya moto 44,946. Hadi kufikia Machi 2024 Mamlaka imekagua jumla ya vyombo vya moto 54,220 Unguja na Pemba sawa na asilimia 120 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 80 ya mwaka. Kati ya vyombo hivyo, 47,149 vimekaguliwa Unguja na 7,071 vimekaguliwa Pemba. Kiambatanisho namba 9A kinahusika.

b. **Utoaji wa Ruhusa za Njia na Usafirishaji:** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ilipanga kutoa ruhusa za njia na usafirishaji 20,324 na kwa kipindi cha miezi tisa ilipanga kutoa ruhusa za njia na usafirishaji 15,243. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya ruhusa za njia na usafirishaji 15,824 kwa gari mbalimbali zinazotoa huduma za usafirishaji wa abiria na mizigo zimetolewa Unguja na Pemba sawa na asilimia 103 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 78 ya makadirio ya mwaka. Kati ya ruhusa hizo 13,508 zimetolewa Unguja na ruhusa 2,316 zimetolewa Pemba. Kiambatanisho namba 9B kinahusika.

c. **Utoaji wa Leseni kwa Gari za Biashara:** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ilipanga kutoa leseni 14,208 kwa gari za biashara na kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2024 imepanga kutoa leseni 10,653 kwa Unguja na Pemba. Hadi kufikia Machi 2024 jumla ya leseni 11,153 zimetolewa kwa gari za biashara aina mbalimbali zinazotoa huduma ya usafirishaji wa abiria na mizigo sawa na asilimia 104 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 78 ya makadirio ya mwaka. Kati ya leseni hizo, leseni 9,653 zimetolewa Unguja na leseni 1,500 zimetolewa Pemba.

d. **Majaribio ya Madereva:** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ilipanga kuwafanyia majaribio ya nadharia na vitendo jumla ya madereva 13,509 na kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 ilipanga kuwafanyia majaribio madereva 10,139 Unguja na Pemba. Hadi kufikia Machi 2024, Mamlaka imefanikiwa kuwafanyia majaribio ya nadharia na vitendo jumla ya madereva 9,864 sawa na **asilimia 97** ya makadirio ya miezi tisa na **asilimia 73** ya makadirio ya mwaka. Madereva 8,188 wamefanyiwa majaribio Unguja na madereva 1,676 wamefanyiwa majaribio Pemba.

e. **Utoaji wa Beji za Utingo na Madereva:** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ilipanga kutoa beji za utingo na madereva wa vyombo vya biashara aina mbalimbali 12,312 na kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 ilipanga kutoa beji za utingo na madereva wa vyombo vya moto 9,234 Unguja na

Pemba. Hadi kufikia Machi 2024 Jumla ya beji 8,047 zimetolewa kwa utingo na madereva wa vyombo vya biashara aina mbalimbali Unguja na Pemba sawa na **asilimia 87** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 65 ya makadirio ya mwaka. Kati ya beji hizo, 7,188 zimetolewa Unguja na 859 zimetolewa Pemba. **Kiambatanisho namba 9C kinahusika.**

f. **Utoaji wa Leseni za Madereva Wanafunzi (Learner Licences):** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ilipanga kutoa leseni za kujifundishia vyombo vya moto kwa madereva wanafunzi 24,148 na kwa kipindi cha miezi tisa ilipanga kutoa leseni 18,111. Hadi kufikia Machi 2024 jumla ya leseni za madereva wanafunzi 15,950 zimetolewa Unguja na Pemba sawa na asilimia 80 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 66 ya makadirio ya mwaka. Kati ya leseni hizo, 14,516 zimetolewa Unguja na 1,434 zimetolewa Pemba.

g. **Utoaji wa Vibali kwa Madereva Wageni:** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ilipanga kutoa vibali 27,320 kwa madereva wageni na kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 ilipanga kutoa vibali 20,493 Unguja na Pemba. Hadi kufikia Machi 2024 Jumla ya vibali 20,071 vya ruhusa ya kuendesha vyombo vya moto kwa wageni vimetolewa Unguja na Pemba sawa na **asilimia 98** ya makadirio ya miezi tisa na asilimi 73 ya makadirio ya mwaka. Kati ya vibali hivyo 19,989 vimetolewa Unguja na 82 vimetolewa Pemba.

**Mapato na Matumizi**

64. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani ilikadiria kukusanya jumla ya TSH 4,387,679,000 Unguja na Pemba. Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, ilikadiria kukusanya jumla ya **TSH 3,290,759,250** na hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **TSH 3,608,136,993** zimekusanywa sawa na asilimia 109 ya makadirio ya miezi tisa na **asilimia 82** ya makadirio ya mwaka.

65. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Mamlaka ya ilipanga kutumia jumla ya **TSH 2,264,225,500** Unguja na Pemba ikiwa **TSH 1,004,654,500** ni kwa kazi za kawaida na **TSH 1,259,571,000**

ni mshahara. Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **TSH 1,697,010,805** zimetumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida na mshahara sawa na **asilimia 75** ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo, **TSH 957,538,280** ni mshahara n**a TSH 739,472,525** ni matumizi ya kawaida. Aidha, katika kipindi hicho Jumla ya **TZS 1,440,000,000** zimewasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali ikiwa ni mchango wa Mamlaka kwenda Serikali Kuu.

**MALENGO YA MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

**66.** **Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Zanzibar itaendelea kutoa huduma za usafiri barabarani ikiwemo kuwafanyia majaribio ya udereva madereva, utoaji wa leseni za madereva wanafunzi, kutoa vibali kwa madereva wageni, kutoa leseni kwa vyombo vya Biashara, kutoa ruhusa za njia za usafirishaji, pamoja na kutoa beji za madereva na utingo.

Vilevile, Mamlaka itaendelea kuimarisha usalama wa watumiaji wa barabara kwa kuwapatia elimu ya usalama barabarani kwa makundi tofauti ya jamii pamoja na kufanya ukaguzi wa njiani ili kubaini wanaokiuka utaratibu.

**67.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na kutekeleza majukumu ya msingi ya utoaji wa huduma za usafiri barabarani na udhibiti wa usalama Barabarani pia imepanga kutekeleza miradi miwili kama ifuatavyo:-

i. Mradi wa Mageuzi ya Utoaji wa Huduma za Mamlaka kwa njia ya Mifumo. (ZARTSA Full Automation System), mradi una lengo la Kuondokana na matumizi ya karatasi katika utoaji wa huduma za Mamlaka, kudhibiti udanganyifu katika upatikanaji wa huduma za usafirishaji.

ii. Ujenzi wa kituo cha kisasa cha ukaguzi wa vyombo vya moto hapa Zanzibar, mradi huu una lengo la kudhibiti usalama wa vyombo ili kupunguza ajali za barabarani.

**Makadirio ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025**

68. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani imekadiria kukusanya jumla ya **TSH 3,698,223,652** kupitia vyanzo vyake mbalimbali na imepanga kutumia jumla ya **TSH 3,208,809,450** kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, **TSH 1,296,860,058** ni matumizi mengineyo na **TSH 1,911,949,392** ni mshahara.

**D.2. MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI ZANZIBAR**

69. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka Usafiri na Usalama Barabarani ina jukumu la kusimamia, kudhibiti na kuendeleza Sekta ya Usafiri wa Baharini. Miongoni mwa kazi zake ni: Usajili wa meli, Usimamizi na udhibiti wa ulinzi na usalama wa meli na bandari, Usimamizi wa uchafuzi wa mazingira ya bahari yatokanayo na meli, Utoaji wa leseni kwa vyombo vidogo vidogo vya baharini, Ukaguzi wa meli na vyombo vidogo vidogo, Uchunguzi wa ajali za baharini, Usimamizi na udhibiti wa huduma za bandari na meli, Usimamizi wa ustawi na maslahi ya mabaharia, Uratibu wa utafutaji na uokozi baharini, Ukaguzi wa meli za kigeni zinapokuwa katika bandari za Zanzibar, Utoaji wa vyeti, leseni, vibali, vitambulisho pamoja na vitabu vya kumbukumbu za mabaharia.

70. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai – Machi 2024, Mamlaka ya Usafiri Baharini imefanikiwa kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo: -

a. **Usajili wa Meli za Kimataifa na Meli za Ndani:** Kwa kipindi cha Julai - Machi, 2024 Mamlaka ilikadiria kusajili jumla ya meli 246 na hadi kufikia mwezi wa Machi, 2024 imefanikiwa kusajili jumla ya meli 257 zenye uzito 'gross tonnage' (GT) wa 590,491 sawa na **asilimia 104** ya makadirio. Kati ya hizo, meli 246 ni usajili wa meli za kimataifa zenye GT 577,560 na meli 11 ni usajili wa ndani zenye GT 12,731.

b. **Usajili wa Vyombo Vidogo vidogo:** Kwa kipindi cha Julai - Machi, 2024 Mamlaka ilikadiria kusajili jumla ya vyombo vidogo vidogo 800, hadi kufikia mwezi wa Machi, 2024 Mamlaka imefanikiwa kusajili jumla ya vyombo vidogo vidogo 1,521 sawa na **asilimia 190** ya makadirio.

c. **Vitabu vya Ubaharia (Discharge Book):** Katika kipindi cha Julai - Machi, 2024 Mamlaka ya Usafiri Baharini ilikadiria kutoa jumla ya vitabu 800 vya ubaharia. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2024 imefanikiwa kutoa jumla ya vitabu 836 vya ubaharia sawa na **asilimia 104** ya makadirio.

d. **Kuthibitisha Mikataba na Vyeti vya Mabaharia Wanaosafiri Nje ya Nchi:** Kwa kipindi cha Julai – Machi 2024, Mamlaka ilikadiria kuthibitisha jumla ya mikataba 290 kwa mabaharia wanaosafiri na meli za nje kupitia kampuni ya DANAOS. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2024, imethibitisha mikataba 406 sawa na **asilimia 140** ya makadirio. Vilevile, Mamlaka ilikadiria kuthibitisha vyeti 220, vya 'ship security awareness' hadi kufikia mwezi wa Machi 2024, jumla ya vyeti 387 vilithibitishwa sawa **na asilimia 176** ya makadirio.

e. **Kuthibitisha Vyeti vya Mabaharia wa Kigeni:** Kwa kipindi cha Julai – Machi 2024, Mamlaka ilikadiria kuthibitisha vyeti vya mabaharia (certificate of competence) 760 kwa mabaharia wa kigeni wanaopanda meli za nje. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2024 jumla ya vyeti 701 vilithibitishwa sawa na **asilimia 92** ya makadirio.

f. **Kutoa Leseni na Vibali kwa Huduma za Usafiri wa Baharini na Bandarini:** Kwa kipindi cha Julai – Machi, 2024, Mamlaka ilikadiria kutoa leseni/vibali 222 kwa Taasisi zinazotoa huduma za usafiri baharini na bandarini. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2024 jumla ya leseni/vibali 167 zimetolewa sawa na **asilimia 75** ya makadirio.

g. **Kutayarisha Kanuni na Miongozo ya kufanyia kazi.** Katika kipindi cha Julai Machi, 2024, Mamlaka ya Usafiri Baharini ilipanga kutayarisha jumla ya kanuni 5 na miongozo 20 kwa ajili ya kufanyia kazi. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2024 Mamlaka ilitayarisha jumla ya kanuni 3 sawa na **asilimia 60** na miongozo 16 sawa na **asilimia 80** ya makadirio.

h. **Kuwajengea Uwezo Wafanyakazi wa Mamlaka.** Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2024, Mamlaka ya Usafiri Baharini ilipanga kuwajengea uwezo wafanyakazi 27 kwa kuwapatia mafunzo katika fani mbali mbali ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Hadi

kufikia mwezi wa Machi 2024 jumla ya Wafanyakazi 27 wamepatiwa mafunzo ya fani mbali mbali sawa na asilimia 100 ya makadirio. Kati ya hao, wafanyakazi (17) walipatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani mbalimbali na wafanyakazi (10) walipatiwa mafunzo ya muda mrefu.

i. **Ukaguzi wa Meli.** Kwa kipindi cha Julai – Machi 2024**,** Mamlaka ilipanga kuzifanyia ukaguzi meli 60 na hadi kufikia mwezi wa Machi, 2024 imefanikiwa kuzikaguwa meli 51 za ndani sawa na asilimia 85. zenye jumla ya GT 41,909. Kati ya meli hizo, meli 34 zenye jumla ya GT 25,373 zilifanyiwa ukaguzi wa kiusalama wa mwaka, meli tisa (9) zenye GT 5,231 zilifanyiwa ukaguzi wa kushtukiza, meli 5 zenye GT 6,821 zilifanyiwa ukaguzi wa awali, na meli 3 zenye GT 4,457 zilifanyiwa ukaguzi chelezoni Mombasa.

j. **Marekebisho ya Sheria.** Mamlaka ya Usafiri Baharini imefanikiwa kutayarisha Rasimu ya marekebisho makubwa ya Sheria ya Usafiri Baharini namba 5 ya mwaka 2006 (Maritime Transport Act No.5, 2006). Kwa sasa Sheria hiyo imeshapelekwa katika Kamati ya Katiba na Sheria ya Baraza la Wawakilishi. Marekebisho hayo ni moja ya miongoni mwa hatua za kurekebisha mapungufu makubwa ya sheria hiyo yalioanishwa katika ripoti ya ukaguzi wa IMO mwaka 2019.

k. **Ukusanyaji wa Mapato:** Mamlaka ya Usafiri Baharini kwa kipindi cha miezi tisa (Julai – Machi, 2024) imefanikiwa kuongeza ukusanyaji wa mapato, ambapo jumla ya **TSH 4,799,472,705** zimekusanywa kwa kipindi hicho ukilinganisha na jumla ya **TSH 3,718,109,057** zilizokusanywa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo kuna ongezeko la jumla ya **TSH 1,081,363,645.**

l. **Kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali:** Mamlaka ya Usafiri Baharini imefanikiwa kujiendesha wenyewe bila ya kutegemea ruzuku kutoka Serikalini. Aidha, kwa kipindi cha Julai - Machi, 2024 Mamlaka imefanikiwa kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali jumla ya **TSH 663,247,415** ikiwa ni **asilimia 25** ya makusanyo ya usajili wa meli za Kimataifa. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Mamlaka ya Usafiri Baharini ilipanga kuchangia Serikali kuu jumla ya **TSH 800,000,000.**

**Mapato na Matumizi**

**71. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Usafiri Baharini kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ilikadiria kukusanya jumla ya **TSH 6,483,983,836** kupitia vyanzo vyake vya mapato. Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 Mamlaka ilikadiria kukusanya jumla ya **TSH 4,812,590,005.** Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **TSH 4,799,472,705** zimekusanywa sawa na asilimia 99.7 ya makadirio ya kipindi cha miezi tisa na asilimia 74 kwa makadirio ya mwaka.

Kwa upande wa matumizi, Mamlaka ya Usafiri Baharini kwa mwaka wa fedha 2023/2024, ilipanga kutumia jumla ya **TSH 6,308,090,400** kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **TSH 3,419,426,677** zimetumika sawa na asilimia 54 ya makadirio ya bajeti kwa mwaka. Kati ya fedha hizo, **TSH 1,397,621,720** ni mshahara na **TSH 2,021,804,957** ni matumizi mengineyo.

**MALENGO YA MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025.**

**72. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Usafiri Baharini kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imepanga kusajili jumla ya Meli 16 za ndani na 240 za kimataifa, kutoa jumla ya leseni 1,500 kwa vyombo vidogo vidogo, vitabu 1,500 vya Mabaharia (Discharge Books), kuthibitisha mikataba 500 ya Mabaharia, kuthibitisha vyeti 480 vya mafunzo ya ulinzi melini (Maritime Security awareness) kwa Mabaharia wanaosafiri na meli za nje kupitia kampuni ya DANAOS, kutoa vitambulisho vya mabaharia (Seafares ID ) 2,000 na kuthibitisha vyeti 960 vya mabaharia wa kigeni (Endorsements). Vilevile, Mamlaka imepanga kutoa Leseni 377 zinazohusu huduma za Usafiri wa Baharini na bandarini, kufanya Ukaguzi wa Meli 89, Kuwajengea uwezo wafanyakazi 43 wa Mamlaka, na kupitia sheria 1 ya ZMA Act No.3 of 2009, kutayarisha Kanuni 5 na miongozo 4 (Standard Operation Procedures - SOP) ya kufanyia kazi.

Pia, Mamlaka ya Usafiri Baharini imepanga kukiimarisha kitengo cha Kusimamia wakaguzi wa meli za nje (ROs), kuanzisha na kuijengea uwezo

Idara ya usimamizi wa mafunzo ya mabaharia kwa kuwapatia mafunzo watendaji na kutayarisha miongozo ya utendaji, kuimarisha usalama wa michezo ya kitalii baharini kwa kushirikiana na Mamlaka husika, kuanzisha na kukipa uwezo kitengo cha kusimamia Chuo cha Mabaharia pamoja na kuongeza mapato yatokanayo na usajili wa meli za Kimataifa ili kuongeza gawio Serikalini.

**Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2024/2025**

**73.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Mamlaka ya Usafiri Baharini imekadiria kukusanya jumla ya **TSH 7,938,815,140** na imepanga kutumia jumla ya **TSH 7,428,993,487** kwa matumizi ya kazi za kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo, jumla ya **TSH 2,395,602,602** ni mshahara, **TSH 5,033,390,885** kwa kazi za kawaida.

**D.3. MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR**

**74.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar ina jukumu la kuviendesha, kuvisimamia na kuvitunza viwanja vya ndege vya Serikali pamoja na kusimamia usalama wa safari za abiria, ndege na mizigo katika viwanja vya ndege vya Serikali. Aidha, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege wakati wa utekelezaji wa majukumu yake inazingatia taratibu na sheria zote za uendeshaji wa viwanja kama zinavyoelekezwa na Tanzania Civil Aviation Authority (TCAA) na International Civil Aviation Organization (ICAO).

**75.** **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imefanikiwa kutekeleza yafuatayo: -

a. **Kuhudumia Safari za Ndege, Abiria na Mizigo:** Mamlaka ya Viwanja vya Ndege iliendelea kutekeleza kazi zake za kawaida za kuhudumia safari za ndege, abiria na mizigo katika viwanja vya Ndege Unguja na Pemba. Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, jumla ya safari za ndege 54,527 zimehudumiwa sawa na **asilimia 72** ya makadirio ya safari 75,321 zilizopangwa kuhudumiwa katika kipindi

hicho. Kati ya safari hizo, safari za ndege 50,056 zilihudumiwa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abedi Amani Karume na safari za ndege 4,471 zilihudumiwa katika Uwanja wa Ndege wa Pemba. Safari za ndege za Kimataifa zilikuwa ni 10,785 na safari za ndani zilikuwa ni 43,742. **Kiambatanisho namba 10 A kinahusika.**

Kwa upande wa huduma za Ndege, Mamlaka imehudumia jumla ya Mashirika na Kampuni za ndege 79 za ndani na nje katika Viwanja vya Ndege vya Zanzibar katika kipindi cha miezi tisa. **Kiambatanisho namba 10 B kinahusika**.

Aidha, jumla ya abiria 1,775,668 wamehudumiwa sawa na ongezeko la asilimia 23 ya makadirio ya abiria 1,438,109 waliopangwa kuhudumiwa kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2024, kati ya hao, Abiria, 1,702,361 walihudumiwa katika Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Abedi Amani Karume na abiria 73,307 walihudumiwa katika Uwanja wa ndege wa Pemba. Kati ya abiria hao, abiria 1,071,409 ni wa safari za kimataifa na abiria 704,259 ni wa safari za ndani. Jumla ya Abiria waliopita (transit passengers) ni 154,540 ikiwa abiria 154,313 walipita katika Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Abedi Amani Karume na abiria 227 walipita katika Uwanja wa ndege wa Pemba. **Kiambatanisho namba 10 C kinahusika.**

Kwa upande wa mizigo, jumla tani 3,074 zilihudumiwa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume sawa na asilimia 82 ya tani 3,730 zilizokadiriwa kwa kipindi cha miezi tisa.

b. **Kuimarisha Ulinzi na Usalama wa Viwanja vya Ndege Unguja na Pemba:** Katika kuimarisha ulinzi na usalama wa Viwanja vya Ndege, kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imefanikiwa kujenga ukuta wa zege wenye urefu wa kilomita moja (km1) pamoja na kuzungushia uzio wa waya (security fence) katika ukuta huo uliozunguka Uwanja wa AAKIA. Pia imefanikiwa kuwapatia mafunzo ya ulinzi na usalama wafanyakazi 84, mafunzo hayo yametolewa katika fani tofauti kama ifuatavyo:- wafanyakazi 5 wamepatiwa mafunzo ya risk assessment, 3 crisis management, 45

screener refreshers, 3 instructors, 5 quality management system, 5 internal audits, 4 wildlife management, 4 safety management system, 3 apron management system, 4 behavioral detection course na 3 air cargo and mails. Lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha wafanyakazi wa Mamlaka kutoa huduma bora.

c. **Utanuzi wa Jengo la Abiria:** Ujenzi wa Jengo Jipya la Pili la Abiria (TB2) umetokana na uchakavu wa miundominu kwenye jengo la pili la Abiria (TB2) hali inayopelekea malalamiko mengi ya watumiaji wa jengo hilo. Serikali imeshaingia mkataba na Kampuni ya Esteem Enterprises kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo na tayari awamu ya mwanzo ya ujenzi wa jengo hilo umeanza rasmi mwezi Januari, 2024, aidha ujenzi wa jengo hilo unatarajiwa kukamilka ndani ya miezi 18. Vilevile katika ujenzi huo Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imelazimika kuvunja baadhi ya majengo na maeneo katika jengo hilo, kati ya maeneo yaliyovunjwa ni eneo linalotumika na abiria wanaotumia ndege za ndani (General Aviation). Ili kuhakikisha watumiaji wa ndege za ndani wanapata huduma bora, Serikali imejenga ukumbi mpya wenye ukubwa wa mita za mraba 628 maalumu kwa ajili ya abiria wanaotumia ndege hizo.

d. **Ujenzi wa Kituo cha Biashara (business center) katika Jengo la Terminal 3:** Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imefanikiwa kuimarisha mazingira ya biashara katika Uwanja wa AAKIA kwa kuingia mkataba na Kampuni ya Estim Enterprise kwa ajili ya kujenga na kuendesha kituo cha biashara (business center) katika Uwanja wa AAKIA. Aidha ujenzi huu utajumuisha maofisi, huduma za mabenki, maduka na mikahawa, kwa sasa mkandarasi tayari ameshawasilisha michoro na ujenzi umeanza na upo katika hatua za awali.

e. **Ukarabati wa Kumbi za Wageni Mashuhuri na Viongozi Wakuu wa Nchi katika Jengo la Abiria la Terminal 1:** Ujenzi wa kumbi za Wageni Mashuhuri (VIP na VVIP) umeanza rasmi mwishoni mwa Mwezi wa Machi, 2024 na utachukuwa muda wa miezi tisa hadi kukamilika kwake. Kwa ujumla kazi za ujenzi zinaendelea vizuri.

f. **Kuimarisha Huduma za Zimamoto na Uokozi Unguja na Pemba:** Katika kuimarisha utoaji wa huduma za zimamoto na uokozi kiwanjani, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imefanikiwa kutoa mafunzo ya zimamoto na uokozi kwa wafanyakazi wake pamoja kufanya zoezi kamili la uokoaji (full emergency exercise) la kujiweka tayari iwapo kutatokea ajali ya ndege, ambalo halikuwahi kufanyika kwa zaidi ya miaka 14 iliyopita.

g. **Kuimarisha Huduma katika Majengo ya Abiria Unguja na Pemba pamoja na kuwapatia Mafunzo ya Uendeshaji na Usimamizi wa Uwanja Wafanyakazi wa Mamlaka Pemba:** Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imefanikiwa kuimarisha huduma katika majengo ya abiria Unguja na Pemba kwa kuwapatia mafunzo wafanyakazi wake ili kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yao., jumla ya wafanyakazi 13 wamepatiwa mafunzo ya muda mafupi ya aina mbalimbali. kati ya hao, 4 wamepatiwa mafunzo ya screener refreshers, 1 crisis management, 1 internal audits, 1 wildlife management, 1 safety management system, 3 air cargo and mails na 2 behavior detections.

h. **Kupata Alama "A" kwenye Ukaguzi wa Masuala ya Ulinzi na Usalama:** Mamlaka imefanikiwa Kupata Alama "A" kwenye ukaguzi wa masuali ya ulinzi na usalama wa viwanja vya ndege uliofanywa na wakaguzi kutoka Shirika lenye dhamana ya Usimamizi wa Usafiri wa Anga Duniani - ICAO kwa kiwanja cha AAKIA.

i. **Kupata Tunzo mbalimbali kwa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abedi Amani Karume (AAKIA):** Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Kiwanja cha AAKIA kimefanikiwa kupata tunzo ya Uwanja Bora wa Ndege Barani Afrika unaotoa huduma bora kwa abiria chini ya milioni mbili kwa mwaka (Best Airport Under 2 Million Passengers in Africa) zinazotolewa na Baraza la Kimataifa la Viwanja vya Ndege (Airport Council International – ACI) zilizotangazwa rasmi siku ya Jumatatu ya tarehe 11 Machi 2023 katika mtandao wa Baraza hilo ambapo tunzo hiyo inatarajiwa kukabidhiwa tarehe 25 Septemba 2024 katika Mkutano na Maonesho ya kila Mwaka ya Huduma kwa Wateja Duniani (World's Annual Customer Experience Summit and Exhibition)

yatakayofanyika huko Atlanta nchini Marekani. Aidha, uwanja huo pia ulipata tuzo ya kiwanja bora kilichofanya mabadiliko makubwa katika huduma ya vyakula na vinjwaji katika jengo la tatu la abiria la uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Amani Abeid Karume (AAKIA), Tunzo hiyo ilitolewa Septemba 2023 huko Bangkok nchini Thailand katika Mkutano unaofanyika kila mwaka wa "Airport Food & Beverage (FAB) +Hospitality ' Conference & Awards". Vilevile, Serikali kupitia mamlaka ya Viwanja vya ndege imeshinda kinyanganyiro cha kuwa mwenyeji wa kongamano la maendeleo ya sekta ya anga (AVIA DEV) linalojumuisha wadau mbalimbali wa sekta ya Anga na Utalii duniani ambalo linatarajiwa kufanyika Zanzibar mwezi Juni 2025. Kongamano hilo litatoa fursa ya Zanzibar kujitangaza duniani pamoja na kuchochea maendeleo ya sekta ya utalii na biashara.

j. **Ujenzi wa Kituo Kipya cha Kutoa Huduma za Mafuta ya Ndege (Fuel Farm):** Uwanja wa ndege wa AAKIA kwa sasa una kituo kimoja cha kutolea huduma za mafuta ya ndege. Mamlaka imeamua kuongeza vituo vyengine vitatu kwa ajili ya kuweka ushindani wa utoaji wa huduma na unafuu wa bei kwa mashirika ya ndege na watumiaji kwa ujumla. Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Kampuni ya Oilcom imeanza ujenzi wa matenki ya mafuta matatu ambapo kila moja litachukuwa takribani lita laki tano ,tenki moja la maji la lita laki tano na ishirini elfu, jengo la ofisi pamoja na miundombinu yote inayohusiana na Zimamoto na Uokozi. Ujenzi wa kituo hicho cha huduma ya mafuta ya ndege unaendelea na unatarajiwa kukamilka mwezi Julai, 2024.

### Mapato na Matumizi

76. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar ilikadiria kukusanya jumla ya **TSH 42,183,292,873** na kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 ilikadiria kukusanya jumla ya **TSH 35,132,733,756** kupitia vyanzo vyake vya ndani. Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **TSH 32,122,215,891** zimekusanywa sawa na **asilimia 91.4** ya makadirio ya miezi tisa na **asilimia 76.1** ya makadirio ya mwaka.

**77. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa matumizi, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar ilipanga kutumia jumla ya **TSH 38,897,172,670** kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo. Kati ya fedha hizo, **TSH 11,573,671,426** ni kwa matumizi mengineyo, **TSH 10,366,754,844** ni mshahara na **TSH 16,956,746,400** kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2024, jumla ya **TSH 27,952,371,049.82** zimetumika sawa na **asilimia 71.8** ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo **TSH 8,442,352,531.46** ni mshahara, **TSH 10,405,959,275.61** ni matumizi mengineyo na **TSH 9,104,059,242.75** ni kwa kazi za maendeleo. Aidha kiasi cha **TSH 22,147,325,696.00** ambazo zimetokana na mkopo kutoka Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) pamoja na mchango kutoka Serikalini zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya la abiria la TB 2.

**MALENGO YA MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

**78. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imepanga kuendelea kuimarisha ulinzi na usalama ili kukidhi viwango vya kitaifa na kimataifa kwa kuvifanyia matengenezo vifaa vya ulinzi na usalama pamoja na kuwapatia mafunzo ya ulinzi na usalama wafanyakazi 217 wa kitengo cha ulinzi na usalama.

**79. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Mamlaka imepanga kuimarisha miundombinu kwa kulifanyia matengenezo makubwa jengo la utawala la Mamlaka (Terminal Building 1) linalotumika sasa, kuendelea na ujenzi wa jengo jipya la abiria (Terminal Building 2) katika uwanja wa AAKIA, ujenzi wa barabara inayozunguka uwanja wa AAKIA kwa ajili ya kufanyia doria, kuimarisha miundombinu ya biashara kwa kujenga kituo kipya cha biashara (Bussiness Centre) katika jengo la abiria la *Terminal Building 3* .

Aidha, katika kuendeleza Uwanja wa ndege wa Nungwi, Serikali imeingia hati ya makubaliano na Kampuni ya INTEX kutoka Kenya kwa lengo la kufanya Upembuzi Yakinifu ya uendelezaji wa Uwanja wa Ndege wa Nungwi.Baada kukamilika kazi hiyo majadiliano ya ujenzi yataanza. Aidha, Mamlaka imepanga kujenga jengo jipya la utawala la ofisi kuu

za Mamlaka, kuweka taa mpya za kuongozea ndege (Approach light) katika maeneo ya barabara ya kuruka na kutua ndege katika uwanja wa AAKIA, kuanza hatua za awali za ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Paje na kununuwa gari la kuzimia moto pamoja na gari la wagonjwa. Kwa upande wa abiria, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imekadiria kuhudumia abiria 2,123,874, Ndege 77,897 na Mizigo tani 3,474 katika Viwanja vyake vya Ndege vya Unguja na Pemba.

**Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2024/2025**

**80. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imekadiria kukusanya jumla ya TSH 51,508,339,680 kupitia vyanzo vyake vya mapato na imepanga kutumia jumla ya **TSH 51,508,339,680**. Kati ya fedha hizo, **TSH 33,663,818,680** kwa kazi za kawaida na **TSH 17,844,521,000** kwa kazi za maendeleo.

**D.4. SHIRIKA LA BANDARI LA ZANZIBAR**

**81. Mheshimiwa Spika,** Shirika la Bandari limepewa jukumu la kutoa huduma za uingizaji na utoaji meli katika Bandari za Unguja na Pemba, ufungaji na ufunguaji wa meli kwenye gati, uangalizi wa alama za kuongozea usafiri wa meli (minara na maboya), uteremshaji na upakiaji wa bidhaa kwenye meli pamoja na vyombo vyengine vya usafiri wa baharini.

**82. Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 Shirika la bandari limefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

a. **Kuhudumia Vyombo, Mizigo na Makontena:** Shirika lilipanga kuhudumia vyombo, mizigo, abiria na makontena katika bandari zake za Unguja na Pemba. Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, Shirika limehudumia vyombo mbali mbali vya mizigo na abiria katika Bandari zake. Jumla ya meli za Kigeni 39 (GRT 580,385) zimehudumiwa sawa na **asilimia 93** ya meli 42 (GRT 600,426) zilizopangwa kuhudumiwa katika kipindi hicho. Aidha, Meli za ndani zilizohudumiwa ni 4,878 sawa na **asilimia 94** ya meli 5,200 zilizopangwa kuhudumiwa. Aidha, Shirika limehudumia majahazi na maboti ya vyuma 6,317 sawa na **asilimia 94** ya majahazi na maboti ya vyuma 6,712 yaliopangwa kuhudumiwa.

Kwa upande wa huduma za mizigo, Shirika limehudumia jumla ya tani 491,422 za mizigo ya meli na majahazi ikiwa ni sawa na **asilimia 85.92** ya tani 572,000 za mizigo zilizopangwa kuhudumiwa.

Aidha, Shirika limehudumia makontena 15,323 (Teus 20,497) sawa na asilimia 115.9 ya makadirio ya makontena 13,215 (Teus 14,209) yaliyopangwa kuhudumiwa katika kipindi hicho. Pia, Shirika lilipanga kuhudumia tani 165,000 za mafuta ya kuwasha (Petrolium product) na hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya tani 131,933 zimehudumiwa sawa na asilimia 80 ya makadirio kwa kipindi hicho.

b. **Uimarishaji wa Bandari ya Mkokotoni:** Shirika limepanga kuimarisha Bandari ya Mkokotoni awamu ya pili kwa kujenga ghala la kuhifadhia mizigo, jengo la kupumzikia abiria, njia ya waenda kwa miguu pamoja na njia ya kuingia na kutoka meli (Approaching Channel). Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 kazi zilizofanyika ni ujenzi wa Jengo la Abiria lenye uwezo wa kuchukua abiria 250, ghala la kuhifadhia mizigo pamoja na ujenzi wa njia ya kupita abiria wakati wa kuelekea kwenye chombo. Kwa ujumla mradi huu umekamilika kwa asilimia 100 kwa awamu ya pili na jumla ya TSH 406,194,299 zimetumika. Awamu ya tatu ya mradi huu utajumuisha ujenzi wa ukuta na kufanya tathmini juu ya kujifukia kwa eneo la gati (Bathmetic survey) ili kupunguza changamoto hiyo pamoja na kufanya tathmini ya soko kwa bandari hiyo.

c. **Ujenzi wa Bandari ya Shumba Mjini:** Mradi huu unajumuisha ujenzi wa Gati, ghala la kuhifadhia mizigo, jengo la kupumzikia abiria la ghorofa 2 pamoja na njia ya kuingia na kutoka meli (Approaching Channel) kwa gharama ya TSH 5,772,506,880. Shirika limepanga kuanza ujenzi wa Gati yenye urefu wa mita 45 na upana wa mita 20 na itakuwa na uwezo wa kuhudumia meli zenye uzito wa GRT (Gross Rated Tonnage) 2000. Kazi za ujenzi zinafanywa na Kampuni ya Comfix & Engineering Smart Solution.

Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 kazi zilizofanyika ni utayarishaji wa eneo la ujenzi, kufanya utafiti wa Maumbile ya Baharini

na Nchi kavu kwa ajili ya kubuni mchoro (Topography and Bathmetric Survey), kufanya utafiti wa Udongo katika Eneo la Baharini (Geotechnical Investigation), usanifu wa mchoro wa gati ambao utatumika kwa ujenzi. Pia Mkandarasi anaendelea kutengeneza matofali makubwa ya zege (blocks) ambayo yataunganishwa ili kujazwa katika upande wa baharini, na kati kati kutajazwa mawe ili kuipa umadhubuti gati (jetty) hiyo na hadi kufikia mwishoni mwa mwezi wa Machi, 2024 jumla matofali (blocks) 135 yametengenezwa kati ya matofali 400 yanayohitajika. Kwa ujumla eneo la mradi lina ukubwa wa Hecta 3.51 sawa na Square meter 35,100 na jumla ya TSH 1,731,752,064 zimetumika kwa ajili ya kumlipa Mkandarasi sawa na asilimia 30 ya gharama za mradi. Mradi huu ulianza rasmi mwezi wa Juni, 2024 na unatarajiwa kukamilika mwezi wa Julai 2024 na kazi za ujenzi zinaendelea.

d. **Uimarishaji wa Bandari ya Mkoani:** Mradi huu una lengo la kuiwezesha Bandari ya Mkoani kuendelea kuhudumia abiria, mizigo pamoja na kuteremsha makontena katika bandari hiyo, ambapo Shirika la Bandari lilifunga Mkataba na Kampuni ya China Railway Bridge Engineering Company Ltd na kazi ya ujenzi ilianza mwezi Septemba 2022 na kukamilika mwezi wa Oktoba 2023 kwa gharama ya TSH. 6,776,745,317.16. Mradi huu umesimamiwa na Mshauri Elekezi Kampuni ya Annova Consultant Company Limited ya Kinondoni Dar es Salaam. Mradi huu umekamilika na kazi zilizofanyika ni :-

- Kujenga sehemu ya kuhifadhi makontena (Container Yard) yenye ukubwa wa mita za mraba 4,200 na uzio wenye mfumo wa usalama wa umeme ambayo ina uwezo wa kuhifadhi makontena 580 kwa kubebesha matatu matatu kwenda juu;
- Kuweka njia ya kupitia abiria yenye urefu wa mita 300 na upana wa mita 2.5, ambayo inakipaa juu ili kuzuia abiria wasirowe au kupigwa na jua;
- Kutanua njia kwa ajili ya kuwezesha vitendea kazi kama Reach Stacker, Crane na Terminal Tractor kupita;
- Kujenga ukuta wa kuzuia mmng’onyoko wa udongo (Retaining Wall) wenye mita 120; na

- Kukarabati gati (Jetty) kwa kuziba nyufa na kurekebisha zege iliyo-haribika.

Aidha, Shirika limepeleka vifaa mbalimbali ikiwemo Reach Staker 2, Crane na Weight bridge kwa ajili ya utoaji wa huduma za makontena ambayo itaanza baada ya kuwasili kwa tug boat na pilot boat ambavyo taratibu za manunuzi ya vifaa hivyo zinaendelea.

Vilevile, Shirika limekamilisha taratibi za ununuzi wa Baji kwa ajili ya Bandari ya Mkoani litakalo wezesha boti za mwendo kasi kufunga gati kwa urahisi katika bandari hiyo. Jumla ya **TSH 3,047,500,000** zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa Baji hilo na linatarajiwa kufika Pemba mwisho wa mwezi wa Juni 2024 likitokea Dubai. Pia katika kuimarisha huduma za bandari hiyo, Serikali imefunga mkataba na muekezaji Fumba Port atakae endesha Bandari ya Mkoani kwa upande wa makontena ambapo itakuwa na uwezo wa kuhudumia makontena 3000 kwa mwaka baada ya kuiboresha.

e. **Bandari ya Wete:** Shirika la Bandari limepanga kuijenga upya bandari ya Wete ili iweze kuhudumia abiria pamoja na mizigo kwa hatua ya awali. Mshauri Elekezi Inros Lackener kutoka Ujerumani anakamilisha kazi ya kufanya upembuzi yakinifu na Usanifu wa awali pamoja na kutayarisha mchoro yakinifu ambao unaonesha mwelekeo mpya wa Bandari hiyo. Hata hivyo, taarifa ya awali ya upembuzi yakinifu huo inaonesha kuwa kunahitajika kuchimbwa ndani ya bahari (dredging ya 6.5m hadi 8.5m), hivyo, Shirika limempa muda wa miezi 3 Mshauri Elekezi bila ya gharama (Extension without cost) kwa ajili ya kukamilisha hatua zilizobakia ikiwemo kuandaa Tender Documents na kuweka mchoro katika hatua tatu za utekelezaji wakati wa ujenzi (Three Phase) ambapo kutachimbwa kwa mita 6. Gharama za mradi ni **TSH 865,271,767.5** ambapo Shirika limeshatumia jumla ya **TSH 458,790,454.5** sawa na **asilimia 53.**

f. **Ujenzi wa bandari ya Fumba:** Ujenzi wa bandari hii ni uwekezaji uliofanywa kwa kuzingatia Matakwa ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 inayotoa nafasi kwa sekta binafsi kuendesha shughuli za bandari ambapo Kampuni hiyo ilipata eneo hilo kupitia Mamlaka ya Uwekezaji

(ZIPA) lenye ukubwa wa hekta 4.96. Kampuni ya Fumba Inland Container Depot Limited imefanya Ujenzi wa bandari kavu (ICD) yenye uwezo wa kuchukua makontena 3000 TEUS pamoja na sehemu ya kulazia lango la meli na ilichukua miezi 3 kukamilika kwake na baadae iliendelea na uwekaji wa mifumo ya kielektroniki ili kuweza kutoa huduma kwa ufanisi. Kwa sasa bandari hiyo imeanza kutoa huduma hiyo ya kushusha makontena. Jumla ya TSH. **Bilioni 17.108** zimetumika katika mradi huu ambapo **TSH. Bilioni 15.3** zimejumuisha ujenzi wa bandari hiyo ambazo zimetolewa na muwekezaji na TSH. Bilioni 1.808 zimetolewa na Serikali kwa ajili ya gharama ya uwekaji wa miundo mbinu ya barabara na umeme. Aidha, ujenzi wa gati utaanza mwezi wa Juni, 2024 na utakamilika ndani ya mwaka mmoja ambapo itajengwa gati yenye urefu wa mita 340 kuingia ndani na meli zenye ukubwa wa mita 225 zitaweza kufunga kwa kina cha maji chenye urefu wa mita 12

g. **Ujenzi wa Bandari ya Kizimkazi:** Shirika linaendelea na matayarisho ya bandari ya kizimkazi baada ya kukamilika zoezi la upimaji na kupata lease ya eneo hilo kutoka Kamisheni ya Ardhi lenye ukubwa wa hekta 23.2. Taratibu za kufanya tathmini ya vipando na majengo zitaanza kwa kushirikiana na Afisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali. Aidha, Kampuni ya ZF DEVCO imesaidia kuandaa Mpango Mkuu wa bandari hiyo ambayo itarahisisha safari za baharini kwa upande wa Kusini Unguja.

h. **Ujenzi wa Bandari ya Abiria Maruhubi:** Shirika linaendelea na matayarisho ya Ujenzi wa Bandari ya abiria Maruhubi ambapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ilitiliana saini Mkataba na ZF DEVCO kwa ajili ya ujenzi wa bandari hiyo ambayo itajengwa mwaka 2024 kwa gharama za **TSH 1,020,000,000,000** sawa na (USD Milioni 400).

   i. **Bandari ya Malindi:** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi chini ya Taasisi yake ya Shirika la Bandari ilifunga mkataba tarehe 18 Mei, 2023 na Afrika Global Logistic (AGL) ambayo imesajiliwa Zanzibar kwa jina la Zanzibar Multipurpose Terminal (ZMT). Mafanikio mbali mbali yamepatikana yakiwemo:-

- Kupungua kwa muda wa kusubiri meli ukutani- kutoka siku 20 – 30 (ZPC) hadi kufikia siku 15 -18 (ZMT),
- Kuongezeka kwa ufanisi katika shughuli za ushushaji na upakiaji wa makontena na mizigo kichele ambapo kwa upande wa makontena ushushaji na upakiaji ilikuwa ni (move) 6 – 8 (ZPC) kwa saa moja hadi kufikia (move) 10 – 12 kwa saa moja (ZMT).
- Kwa upande wa mizigo kichele kutoka tani 1,800 -1,900 kwa masaa 8 (ZPC) hadi kufikia tani 2,200 kwa masaa 8 (ZMT)
- Kufungwa kwa taa za kisasa katika eneo la bandari zenye kurahisisha utoaji wa huduma kwa masaa 24.
- Kujengwa kwa bandari kavu iliyofikia asilimia 50 itakayorahisisha utoaji wa huduma kwa haraka na ufanisi.

Kwa sasa muwekezaji anaendelea na ujenzi wa bandari kavu katika eneo la Maruhubi lenye ukubwa wa hekta 2 ambapo ujenzi umefika asilimia 50 pamoja na kuwasili kwa vitendea kazi mbali mbali ikiwemo Reach Staker 2 na mobile crane ili kufikia lengo la kuleta ufanisi kama inavyotarajiwa na Serikali. Aidha, imewapa mafunzo ya udereva wa zana nzito (Mobile Habour Crane na Reach Staker) watendaji 42 pamoja na vyeti yatakayo wasaidia kuweza kufanya kazi zao kwa ufanisi.

j. **Uimarishaji wa Mifumo ya TEHAMA:** Shirika linaendelea kuweka mifumo ya kielektroniki (E-Port) kwa ajili ya kuimarisha huduma zake na kuongeza ufanisi katika utawala, uendeshaji wa vyombo na uhudumiaji mizigo. Mifumo hiyo inatarajiwa kuongeza ufanisi wa uendeshaji, kupunguza nyakati za kugeuka kwa vyombo "Turn-around time", kupunguza msongamano wa utoaji wa mizigo, kuimarisha ulinzi na kuboresha huduma kwa wateja. Hivyo, Shirika liliingia Mkataba na Kampuni ya "Fortris Company Limited" kutoka Tanzania ikishirikiana na kampuni ya Wartsila Voyage Limited kwa gharama za Dola za Kimarekani Milioni 6,569,143.31 sawa na Bilioni 16.4 fedha za kitanzania. Hadi sasa mkandarasi ameshalipwa asilimia 70 ya fedha hizo ambazo ni sawa na Dola za Kimarekani 4,598,400.317 sawa na Bilioni 11,941,788,314.8 fedha za kitanzania. Mradi huu umeanza mwezi wa Aprili, 2022 na unatarajiwa kukamilika Aprili, 2025.

Mradi wa E-Port una vipengele vitano vikuu katika utekelezaji wake kama ifuatavyo:-

i. **Mfumo wa Kusimamia Matumizi ya Mafuta** "Fleet Fuel Management System (FFMS)": Mfumo huu umekamilika ambapo vifaa vimeshafungwa kwenye vyombo pamoja na kuwekwa kwa kituo maalumu cha uwekaji wa mafuta. Mfumo huu umeanza kufanya kazi na kuokoa upoteaji wa mafuta kwa asilimia 40 ambapo upo chini ya ZMT.

ii. **Mfumo wa Kuendesha Shughuli za Kuondoa Shehena za Bandari** "Terminal Operating Sytem (TOS)". Mfumo huu unasimamia shughuli zote za uendeshaji ndani ya Bandari ikiwa ni pamoja na huduma za "stevedoring" (utoaji wa vifaa na upakiaji), upangaji wa yadi, harakati za kuingiza na kutoa makontena ndani ya bandari, kuendesha harakati za mizigo ndani ya "Yard" ya Bandari na Bandari Kavu "ICD", kusimamia magari yote katika lango kuu la kuingia bandarini na wakati wa kupakia mizigo, kusimamia ukataji wa kontena "seal breaking", kusimamia malipo yote ya ndani pamoja na kutoa "control numbers", kupokea "manifest" kutoka kwa "shipping liners' pamoja na kuchukua taarifa zote za mteja "Clearing and Forwarding Agents". Teknolojia hii inasimamiwa na Wataalamu kutoka Uturuki chini ya Kampuni ya Wartsila. Mfumo huu umekamilika na kukabidhiwa ZMT. Aidha, mfumo huu ulifanyiwa majaribio mwezi wa Juni mwaka jana, kwa sasa unawekwa katika utaratibu wa kimatumizi, mfumo uliokoa fedha za Shirika Milioni 600 kwa mwezi katika kipindi cha majaribio, ambapo ni moja ya mafanikio makubwa katika Shirika kupitia mradi huu.

iii. **Mfumo wa Kusimamia Rasilimali za Taasisi "Enterprise Resources Management (ERP)":** Mfumo huu ni mfumo muhimu kwa kusimamia shughuli za kila siku za Taasisi zikiwemo uhasibu, ununuzi na ugavi, rasilimali watu, marekebisho ya vifaa pamoja na shughuli nyengine zote za kiofisi. Mfumo umekamilika na mafunzo ya utumiaji kwa watendaji wa mfumo huo yameshafanyika. Kwa sasa unafanyiwa marekebisho ya taarifa zinazohusu wafanyakazi.

iv. **Mfumo wa Kuongoza na Ulinzi wa Meli Baharini** "Vessel Traffic System (VTS)" Mfumo huu utatumika kusimamia usalama wa vyombo baharini kwa urefu wa masafa ya zaidi ya "nautical" 50 kuelekea bahari kuu, ambapo utaongoza meli na kuzifuatilia zikiwa baharini hata kama zitakuwa zimezima mitambo yao "silence mode". Mfumo huu utakidhi matakwa ya Sheria za kimataifa zinazosimamiwa na Shirika la Bahari Duniani (IMO). Kwa sasa mfumo wa VTS upo katika asilimia 50 ya utekelezaji wake, baadhi ya vifaa tayari vishafungwa na kufanyiwa "software installation" na vyengine vinatarajiwa kufika Disemba mwaka huu. Aidha, ujenzi wa minara mitatu muhimu unaanza kwa ajili ya kazi hiyo katika maeneo ya Maruhubi, Malindi na Fumba.

v. **Mfumo wa Kutoa Taarifa ya Mifumo mengine pamoja na Kuhudumia Wateja** "Electronic Portal (E-PORTAL)". Mfumo huu unaunganisha mifumo yote iliyotajwa hapo juu ili kutoa taarifa ya pamoja katika sehemu moja (Dash board) ambayo itaonesha viashiria muhimu vya utendaji kazi (KPIs) na shughuli zote za bandari kupitia mifumo mengine.

**Mapato na Matumizi**

83. **Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Shirika la Bandari lilikadiria kukusanya jumla ya **TSH 31,856,681,092.22** kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali na kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 Shirika lilikadiria kukusanya jumla ya **TSH 23,743,925,717.96**. Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **TSH 22,325,802,734.37** zimekusanywa sawa na asilimia 94 kwa makadirio ya miezi tisa na asilimia 70 ya makadirio kwa mwaka.

Kwa upande wa matumizi, Shirika la Bandari kwa mwaka wa fedha 2023/2024 lilipanga kutumia jumla ya **TSH 25,585,019,060.40** kwa kazi za kawaida na **TSH 35,781,908,959.27** kwa kazi za maendeleo. Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 Shirika lilipanga kutumia TSH 18,235,600,000 kwa kazi za kawaida na **TSH 15,651,616,089.22** kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2024, jumla ya **TSH 17,447,298,301.36** zimetumika sawa na **asilimia 96** ya makadirio kwa

kipindi cha miezi tisa na asilimia 68 kwa mwaka kwa kazi za kawaida, na kwa upande wa miradi zimetumika TSH. 12,544,831,250.39 sawa na asilimia 80 kwa kipindi cha miezi tisa na asilimia 35 kwa makadirio ya mwaka.

## MALENGO YA SHIRIKA LA BANDARI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**84. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025 Shirika la Bandari limepanga kuhudumia meli za ndani zipatazo 7,200, meli za kigeni 160 na Majahazi 12,400.

Aidha, kwa upande wa huduma za mzigo, Shirika linatarajia kuhudumia tani 1,881,645 za mzigo mchanganyiko, makontena 68,360 na tani 158,000 za mafuta ya kuwasha (Petroleum Fuel)

**85. Mheshimiwa Spika,** Shirika limepanga kuendelea kukamilisha miradi inayoendelea ambayo ilianza utekelezaji wake katika kipindi cha mwaka wa fedha uliopita, ikiwemo Ujenzi wa Bandari ya Shumba Mjini, Kizimkazi, ujenzi wa Bandari kavu na Uimarishaji wa Bandari ya Mkoani ikiwemo kujenga jengo la Ofisi na jengo la abiria, Ujenzi wa Bandari ya abiria Mpiga Duri na kujenga maeneo ya vituo vya usafiri wa baharini (sea tax).

Aidha, Shirika la Bandari limepanga kufanya ukarabati wa minara ikiwemo mnara wa Makunduchi na Mwana mwana, vilevile, Shirika limepanga kufanya manunuzi mbalimbali ili kuimarisha huduma za bandari, manunuzi hayo ni:- tagi na pailoti boti, gari, mashine ya upekuzi wa mizigo, maboya ya kuongozea meli, vifaa vya Tehama pamoja na vifaa vya kudhibiti umwagikaji wa mafuta baharini (Oil Spill Equipment). Aidha, Shirika limepanga kuwajengea uwezo wafanyakazi 43 kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ili waweze kufanyakazi kwa ufanisi.

### Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2024/2025

**86. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Shirika la Bandari Zanzibar limekadiria kukusanya jumla ya **TSH 37,962,452,234.51** na

kutumia jumla ya **TSH 77,441,297,397.27.** Kati ya fedha hizo, **TSH 8,021,731,452.00** kwa kazi za kawaida, TSH 8,761,006,470.00 mishahara na **TSH60,658,559,475.27** kwa kazi za maendeleo ambapo italazimika Shirika la Bandari kuchukua mkopo wa **TSH 40,000,000,000** ili kuzitekeleza baadhi ya shughuli za miradi.

### D.5. SHIRIKA LA MELI ZANZIBAR

**87. Mheshimiwa Spika,** Shirika la Meli Zanzibar linamilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa asilimia mia moja. Shirika hili lilianzishwa rasmi chini ya Sheria nambari 3 ya mwaka 2013 (The Zanzibar Shipping Corporation Act, 2013) na limepewa jukumu la kuzisimamia na kuziendesha meli zote za Serikali pamoja na kutoa huduma za uwakala kwa meli za kigeni zinazoingia katika bahari ya Zanzibar.

**88. Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 Shirika la Meli limefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

a. **Matengenezo ya Meli ya MV Mapinduzi II:** Shirika la Meli Zanzibar linaendelea kuifanyia matengenezo makubwa MV Mapinduzi II kwa kutumia Kampuni ya Kookje Engineering ya Korea. Mashine zote za meli hiyo zimeshatengenezwa na zinafanya kazi vizuri ambapo kwa sasa matengenezo hayo yameshafikia zaidi ya asilimia 80. Meli hiyo inatarajiwa kupelekwa Chelezoni, Mombasa Kenya tarehe 22 Juni, 2024 kwa ajili ya kutoa na kuisafisha 'shaft', kupakwa rangi chini ya meli na kuangaliwa kama kutakuwa na uhitaji wa matengenezo mengine. Meli hiyo inatarajiwa kutoka chelezoni baada ya mwezi mmoja na inatarajiwa kuanza kazi ndani ya mwezi wa Septemba, 2024.

b. **Utoaji wa Huduma ya Kusafirisha Mafuta kwa Kutumia Meli ya MT Ukombozi II:** Meli ya MT Ukombozi II inaendelea kufanya kazi vizuri ya kusafirisha mafuta kutoka Tanga na Dar es Salaam kuja Zanzibar. Meli hii inaendelea kukodiwa na kwa kodi ya safari (voyage charter) na Kampuni ya GBP Tanzania. Meli ya MT Ukombozi II kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2024 imefanya jumla ya safari 29 sawa na asilimia 74 ya safari 39 zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2023/24. Jumla ya **TZS 3,770,000,000** zimepatikana kutokana na safari hizo.

c. **Utoaji wa Huduma za Uwakala wa Meli:** Shirika linaendelea kutoa huduma za uwakala wa meli ambapo kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya meli 363 za kigeni zimehudumiwa, kati ya meli 301 zilizopangwa kwa mwaka sawa na asilimia 121 ya makadirio. Meli hizo ni pamoja na meli za kuchukua makasha, mafuta na gesi, pamoja na meli za Kijeshi, meli za kuchukuwa kichele na meli za kitalii. Meli hizi zimeongezeka kutokana na kuanza kazi kwa bandari ya Fumba, 'Royal Tour' ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwepo na mahitaji makubwa ya matumizi ya gesi katika nchi za jirani.

d. **Ujenzi wa Boti mbili za Mwendo wa Kasi:** Wizara kupitia Shirika la Meli limeanza utaratibu wa ununuzi wa ujenzi wa boti mbili za mwendo wa kasi zitakazofanya kazi baina ya Unguja, Pemba, Tanga na Dar es Salaam. Ujenzi wa boti hizo unatarajiwa kuanza mwezi wa Julai, 2024 na kukamilika mwezi Machi, 2026.

**Mapato na Matumizi**

**89. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Shirika la Meli Zanzibar lilikadiria kukusanya jumla ya **TSH 12,539,656,218** na hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya **TSH 9,422,431,443** zimekusanywa sawa na **asilimia 75** ya makadirio ya bajeti.

Kwa upande wa matumizi, Shirika lilipanga kutumia jumla ya **TSH 11,472,724,836** kwa kazi za kawaida na **TSH 922,130,000** kwa kazi za Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **TSH 6,415,011,840** zimetumika sawa na asilimia 56 kwa kazi za kawaida na **TSH 423,337,553** zimetumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 46 ya makadirio ya bajeti.

**MALENGO YA SHIRIKA LA MELI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

**90. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Shirika limepanga kuendelea na matengenezo ya meli ya MV Mapinduzi II na kuanza kazi ya kusafirisha abiria 38,400 na mizigo tani 12,000 baina ya Unguja na

Pemba, kujenga boti mbili za mwendo wa kasi ambazo zitafanya kazi ya usafirishaji abiria baina ya Unguja, Pemba, Tanga na Dar es salaam, Kuendelea kutoa huduma za uwakala kwa meli zote zinazokuja katika bahari ya Zanzibar.

Aidha, Shirika limepanga kuwajengea uwezo wafanyakazi wake, kuipeleka meli ya MT Ukombozi II chelezoni Mombasa, Kenya kwa ajili ya ukaguzi pamoja na kuendelea kuyafanyia matengenezo majengo ya Afisi Makao Makuu na Dar es Salaam.

**Makadirio ya Bajeti ya Mwaka wa fedha 2024/2025**

**91.** **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Shirika limepanga kukusanya jumla ya **TSH 14,102,265,605** kupitia vyanzo vyake vya mapato na kutumia 13,829,214,241 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

**D.6. SHIRIKA LA MAWASILIANO (ZICTIA)**

**92.** **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Mawasiliano Zanzibar (ZICTIA) limeanzishwa kwa Sheria nambari 4 ya mwaka 2023 na limepewa jukumu la kusimamia na kuendesha Miundombinu ya Kimkakati ya Mawasiliano ambayo ni Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano wa Zanzibar na Kituo cha Taifa cha Kuhifadhia Taarifa (Data Center).

**93.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 ZICTIA imefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

a. **Kuunganisha vituo vya Taasisi za Serikali na Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano:** ZICTIA imeendelea na kazi za kuviunganisha na Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano vituo vya Taasisi mbali mbali za Serikali (Unguja na Pemba) ambapo kwa kipindi cha miezi tisa (Julai, 2023 hadi Machi, 2024), ilipanga kuviunganisha vituo 57 na Mkonga wa Mawasiliano na hadi kufikia Machi, 2024 ZICTIA imefanikiwa kuviunganisha vituo ishirini na saba (27) Unguja na Pemba sawa na asilimia 47 ya makadirio ya miezi tisa. Vituo hivyo kwa Unguja ni Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) - Mwanakwerekwe, Mazizini na Mpirani,

Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) – Tunguu na Amani, Shirika la Biashara Zanzibar (ZSTC), "Indian Institute of Technology and Madras (IIT Madras)" - Bweleo, Kikosi cha Valantia Zanzibar (KVZ) – Amani Viwandani, Tume ya Ushindani Halali wa Biashara Zanzibar, Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar (eGaz) - Michenzani Mall, Idara ya Misitu - (Jozani na Dole), Nyumba ya Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi Mstaafu - Kizimkazi, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar (ZALIRI), Taasisi ya Usimamizi wa Hospitali za Wilaya – Saateni.

Kwa upande wa Pemba ni Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) - Chake chake na Mkoani, Mamlaka ya Mapato (ZRA), Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar (ZAGPA), Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (OMPR) - Tibirinzi, Ofisi ya Elimu ya Mafunzo ya Amali - Madungu, Tume ya Mipango - Gombani, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ (TAMISEMI) - Machomane, Baraza la Wawakilishi - Wete, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Zanzibar - Gombani, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto - Gombani pamoja na Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar - Wete.

b. **Matengenezo ya Mkonga wa Mawasiliano:** Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, ZICTIA imefanya matengenezo ya Mkonga katika maeneo mbali mbali (Unguja na Pemba). Kwa upande wa Unguja matengenezo hayo yamefanyika eneo la njia ya Bububu Polisi ambapo kazi ya kuzikaza nyaya za Mkonga zilizowekwa juu (Overhead) imefanyika. Matengenezo yaliendelea katika maeneo ya Welezo – Msikiti Makufuli ambapo Mkonga uliharibika kutokana na shoti ya umeme iliyopelekea kubadilishwa kwa Mkonga usiopungua urefu wa mita 700 katika eneo hilo.

   Katika eneo la Bububu kwa Kisasi – Mtoni yamefanyika matengenezo ya mkonga wa juu uliokatwa na gari la mizigo. Matengenezo mengine yalifanyika katika eneo la Mwera baada ya mkonga kuangukiwa na mti. Kazi ya kuuhamisha mkonga kutoka ardhini na kuupitisha kwenye nguzo imeendelea kwa maeneo ya Bububu skuli hadi Kibweni. Vile

vile matengenezo yalifanyika katika njia (Route) ya Paje - Matemwe yaliyosababishwa na mkonga huo kukata huduma. Matengenezo yaliendelea katika Shehia ya Welezo - Karakana kwa kubadilisha nguzo mbovu pamoja na nguzo iliyoanguka katika eneo la Mwanakwerekwe.

Kwa upande wa Pemba matengenezo yalifanyika katika eneo la Munguyupo - Mkoani baada ya mkonga kuharibika kutokana na mmomonyoko wa ardhi uliosabishwa na mvua kubwa. Vile vile, matengenezo yalifanyika Dimbani kutokana na kuanguka kwa nguzo. Aidha, matengenezo yalifanyika katika Shirika la Bandari - Mkoani baada ya kukosekana kwa mawasiliano.

Aidha, Shirika la Mawasiliano limelazimika kuweka njia (route) mpya ya Mkonga wa dharura katika maeneo mbalimbali ya Unguja ili kunusuru kukosekana kwa mawasiliano kunakoweza kusababishwa na miradi ya ujenzi wa barabara inayoendelea nchini. Njia hizo ni Masingini - Dole, Dole – Kijichi, Dole – Mndo na Kisakasaka – Fumba - Nyamanzi. Aidha, ZICTIA imeendelea na uimarishaji wa huduma katika vituo vya mkonga (POP) kwa kuvifanyia maboresho (services) pamoja na kuvifanyia matengenezo vifaa mbali mbali ikiwemo Vipoza hewa (AC) na Majenereta ya vituo vyote Unguja na Pemba.

c. **Kuhifadhi Taarifa za Mifumo katika Kituo cha Kuhifadhia Taarifa ( Data Center):** Katika kipindi cha Julai 2023, hadi Machi, 2024 ZICTIA imeendelea kupokea na kuihifadhi katika Kituo cha Kuhifadhia Taarifa mifumo mipya kutoka katika taasisi mbali mbali. Taasisi hizo ni Wizara ya Afya, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Wakala wa Majengo Zanzibar, Chuo cha Utawala wa Umma (IPA), Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo na vya Kati (SMIDA), Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Tume ya Utumishi Serikalini - Skuli ya Sheria pamoja na Ofisi ya Rais - Ikulu.

d. **Kuwapatia Mafunzo mbalimbali Wafanyakazi:** Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 ZICTIA ilipanga kutoa mafunzo kwa wafanyakazi kumi na tano (15) katika fani tofauti. Hadi kufikia Machi, 2024 ZICTIA imefanikiwa kuwapatia mafunzo wafanyakazi wanne (4)

ambao walihudhuria mafunzo ya muda mfupi katika vyuo mbali mbali nchini kwa lengo la kuwaongezea ufanisi katika maeneo yao ya kazi, ambapo wafanyakazi watatu (3) kati ya hao walipata uelewa juu ya mfumo wa uchambuzi wa taarifa za Kijografia (QGIS and Autocad Services) na mmoja (1) katika mafunzo ya maendeleo ya Ujuzi wa Uhasibu na Udhibiti wa Mapato (Revenue, Accounting and Control Skills Development). Aidha, ZICTIA imeupatia uongozi mafunzo yanayohusu upangaji wa mikakati na mfumo wa usimamizi unaotumika kuboresha utendaji kazini (Balanced score card) ili kuwaongezea uwezo wa utendaji kazi zao. Vile vile, ZICTIA imetoa uelewa kwa wafanyakazi wote juu ya utekelezaji wa majukumu ya taasisi ya Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar (ZHSF) na Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPRA).

e. **Ujenzi wa Kituo Mbadala cha Kuhifadhia Taarifa:** ZICTIA imeanza kutekeleza mradi wa ujenzi wa kituo mbadala cha kuhifadhia taarifa (Tier 3 Data Center) katika maeneo ya uwekezaji wa TEHAMA - Fumba ambapo kwa sasa kazi ya Upembuzi Yakinifu inaendelea na tayari Mshauri Elekezi ameshawasilisha ripoti ya awali kwa ajili ya kupata maoni. Mradi huu unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

f. **Kuufikisha Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano Majumbani:** ZICTIA imepanga kuufikisha Mkonga majumbani kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa huduma nafuu katika matumizi ya TEHAMA. Kazi ya Upembuzi Yakinifu inaendelea kwa mujibu wa mkataba uliosainiwa baina ya ZICTIA na HONORA (TIGO/ZANTEL).

**Mapato na Matumizi**

**94. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Shirika la Mawasiliano Zanzibar lilikadiria kukusanya jumla ya **TSH 7,000,000,000** na kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, ilikadiria kukusanya jumla ya **TSH. 5,075,000,000.00** kupitia vyanzo vyake vya mapato na hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya **TSH. 8,410,993,931** zimekusanywa

sawa na asilimia 166 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 120 ya makadirio ya mwaka. Aidha, ZICTIA imefanikiwa kupata mkopo wa **TSH 4,000,000,000** kutoka Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ).

Kwa upande wa matumizi, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Shirika la Mawasiliano Zanzibar lilipanga kutumia jumla ya TSH 15,343,688,500 na kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, ZICTIA ilipanga kutumia jumla ya **TSH 12,194,733,055**. Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya TSH 9,030,386,807 zimetumika sawa na asilimia 74 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 59 ya makadirio ya mwaka, ikiwa **TSH 859,892,394** ni mshahara, **TSH 2,330,725,291** ni kwa kazi za kawaida na T**SH 5,839,769,122** kwa miradi ya maendeleo.

**MALENGO YA SHIRIKA LA MAWASILIANO ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025.**

**95. Mheshimiwa Spika,** ZICTIA imepanga kuimarisha huduma zilizopo na kuanzisha huduma mpya ikiwemo ya mtandao (Public WiFi) katika maeneo yenye mikusanyiko ya watu kwa malipo ya bei nafuu, kuanza rasmi ujenzi wa Kituo Mbadala cha Kuhifadhia Taarifa (Data Center) katika Maeneo ya uwekezaji Fumba, kulaza mkonga wa baharini (International Gateway) kutoka Mombasa, Kenya - Micheweni, Pemba hadi Fumba, Unguja. Aidha, Shirika la Mawasiliano limepanga kuimarisha njia ya kusafirishia mawasiliano kutoka Unguja hadi Pemba kupitia Minara pamoja na kuandaa Mpango Mkuu (Master Plan) wa uwekaji Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar.

**Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**96. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Shirika la Mawasiliano Zanzibar limekadiria kukusanya jumla ya **TSH 15,877,471,996.** na limepanga kutumia jumla ya **TSH 9,949,359,616** kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo. Ikiwa **TSH 2,074,798,800** ni mshahara, **TSH 7,774,560,816** ni kwa matumizi mengineyo na kazi za maendeleo.

## D.7 BODI YA USAJILI WASANIFU, WAHANDISI NA WAKADIRIAJI MAJENGO

### MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025.

**97. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha, 2024/2025 Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo imekadiria kusajili wataalamu 95 na wasimamizi wa miradi 280 katika fani ya ujenzi wa majengo na kuwaendeleza wataalamu wenye kada za Usanifu, Uhandisi na Ukadiriaji Majengo na wengineo ili waweze kutekeleza kazi zao kwa weledi. Aidha, Bodi imepanga kuwajengea uwezo watendaji wa Bodi kwa kuwapatia mafunzo maalumu ya uelewa wa kazi za Bodi.

Bodi imepanga kufanya ukaguzi wa maeneo 190 kwa wasimamizi wa kazi za ujenzi wa majengo zinazofanywa na Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo katika maeneo yote ya Unguja na Pemba kwa lengo la kupata ujenzi bora na salama.

Aidha, Bodi imepanga kuendeleza programu ya mafunzo ya vitendo (Structure Apprentieceship Program) kwa wahitimu wenye kada zilizotajwa kwenye sheria kwa kuwawezesha kujiunga katika kakampuni zinazofanya kazi za kada zao kwa kushirikiana na Taasisi za nje zinazotoa misaada.

### Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**98. Mheshimiwa Spika,** Mwaka wa fedha wa 2024/2025, Bodi ya Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo imekadiria kukusanya Jumla ya **TSH 530,000,000** kupitia vyanzo vyake vya mapato. **Asilimia 50** ya makusanyo zitatumika kwa ajili ya kazi za Bodi na **asilimia 50** iliyobaki itaingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

### D.8. BODI YA USAJILI WA WAKANDARASI

### MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025.

**99. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha, 2024/2025, Bodi ya Usajii wa Wakandarasi imepanga kuendelea na usajili wa Wakandarasi wapya na kuwapandisha madaraja Wakandarasi ambao walishasajiliwa na Bodi, kuendelea na usajili wa miradi yote ambayo inatekelezwa na wakandarasi hapa Zanzibar, kufanya ukaguzi ili kuhakikisha ujenzi wote unaofanyika nchini unatekelezwa kwa mujibu wa taratibu na sheria za Bodi ya Usajili wa Wakandarasi na unatimiza viwango vya ujenzi vilivyowekwa (standards), kuandaa semina, mikutano na mafunzo mbali mbali kwa Wakandarasi, wadau wa sekta ya ujenzi, Wajumbe na Watendaji wa Bodi ili kuwajengea uwezo katika majukumu yao ya kila siku pamoja na kushajihisha wanafunzi kupenda masomo ya sayansi ili kuwa wataalamu wa fani mbali mbali katika sekta ya ujenzi.

### Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**100. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Bodi ya Usajili wa Wakandarasi imekadiria kukusanya Jumla ya TSH 402,000,000 kupitia vyanzo vyake vya mapato. Asilimia 50 ya makusanyo zitatumika kwa ajili ya kazi za Bodi na asilimia 50 iliyobaki itaingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

## E. MASHIRIKIANO NA TAASISI ZA MUUNGANO

**101. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi imeendelea kushirikiana na Taasisi za Muungano zilizopo hapa Zanzibar katika utoaji wa huduma na usimamizi wa Sekta ya Mawasiliano na Usafirishaji. Miongoni mwa Taasisi hizo ni Mamlaka ya Usafiri wa Anga ya Tanzania (TCAA), Mamlaka ya Hali ya Hewa ya Tanzania (TMA), Mamlaka ya Mawasiliano ya Tanzania (TCRA), Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), Shirika la Huduma za Posta Tanzania (TPC), Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) na Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC).

**102. Mheshimiwa Spika,** Aidha, Wizara inaendelea kushirikiana kwa karibu na Wizara zisizokuwa za Muungano za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo zinashabihiana kimajukumu na kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma katika sekta ya Usafirishaji, Ujenzi na Mawasiliano hapa Zanzibar. Wizara hizo ni:- Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Uchukuzi na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Mashirikiano na Wizara hizi pamoja na Taasisi zake yamechangia sana kukuza Sekta za Ujenzi, Usafiri na Mawasiliano hapa Zanzibar.

Napenda kuchukua nafasi hii kuzipongeza Wizara hizo na Taasisi zake kwa kushirikiana kwa karibu na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi na nachukua fursa hii kuzitaka ziendeleze ushirikiano huo kwa maslahi mapana ya Nchi yetu.

## F. MCHANGO WA SEKTA BINAFSI KATIKA SEKTA YA UJENZI, USAFIRISHAJI NA MAWASILIANO.

**103. Mheshimiwa Spika,** Sekta Binafsi imeendelea kutoa mchango mkubwa katika kusaidia juhudi za Serikali za kuendeleza na kuimarisha huduma za ujenzi na majengo, kuimarisha huduma za usafiri wa Anga, Baharini na Nchi kavu pamoja na huduma za mawasiliano hapa Zanzibar. Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi inatambua na kuthamini mchango wa sekta binafsi katika kujenga uchumi wa nchi yetu kwa kutoa huduma bora zenye kufanikisha sekta nyengine za kiuchumi na kijamii, kuchangia Pato la Taifa na kutoa ajira kwa wananchi. Wizara itaendelea kuhamasisha na kuweka mazingira mazuri ya kisera kwa sekta hizo ili ziendelee kuimarisha huduma za ujenzi, usafiri na mawasiliano hapa Zanzibar.

**104. Mheshimiwa Spika,** nakuchukua nafasi hii kuzipongeza Taasisi binafsi zinazotoa huduma mbalimbali za ujenzi, usafiri na mawasiliano kwa kazi nzuri wanayoifanya na naziomba ziendelee kushirikiana na Serikali katika kuwahudumia wananchi.

## G. MUELEKEO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI KWA KILA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**105. Mheshimiwa Spika,** Baada ya kutoa maelezo ya utekelezaji kwa kila programu zinazosimamiwa na Wizara pamoja na Taasisi zinazojitegemea zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, kwa ruhusa yako sasa, naomba kuwasilisha muelekeo wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

## G.1. VIPAUMBELE VIKUU VYA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**106. Mheshimiwa Spika,** matayarisho ya bajeti hii yamezingatia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar (2050), Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2030, Sera ya Taifa ya Usafiri Zanzibar (2008), Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (2013), Mpango Mkuu wa Usafiri Zanzibar (Zanzibar Transport Master Plan - 2007), Mpango wa Taifa wa Maendeleo Zanzibar - ZADEP (2021- 2026), Sera mbalimbali za sekta mtambuka za Taifa, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2020-2025), Mpango Mkakati wa Wizara (Strategic Plan), Takwimu za matokeo ya Sensa ya Watu na Makaazi ya mwaka 2022, ahadi pamoja na maagizo mbalimbali yaliyotolewa na Viongozi Wakuu wa Kitaifa .

**107. Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia miongozo hiyo pamoja na Ahadi na Maagizo mbalimbali ya viongozi Wakuu wa kitaifa nchi, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025, Vipaumbele vikuu vya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ni :- kuimarisha miundombinu ya bandari, miundombinu ya usafiri wa barabara, miundombinu ya usafiri wa Anga, Miundombinu ya mawasiliano pamoja na kutayarisha Sera, Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali itakayowezesha kusimamia na kutoa huduma bora kwa jamii katika sekta ya Usafirishaji, Ujenzi na Mawasiliano hapa Zanzibar.

## G.2 MUHTASARI WA MAELEZO KWA KILA PROGRAMU NA MALENGO YANAYOTARAJIWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**108. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia Sekta ya Usafirishaji, Ujenzi na Mawasiliano kupitia Programu Kuu nne (4) ambazo ni: - Programu ya Usafirishaji, Programu ya Ujenzi na Majengo ya Serikali, Programu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) pamoja na Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi.

**109. Mheshimiwa Spika,** programu kuu zilizoainishwa katika bajeti hii zimewekewa malengo makhususi, matokeo ya muda mrefu yatakayopatikana, huduma zitakazotolewa, shabaha na viashiria mbalimbali vitakavyotumika kupima utekelezaji wa huduma zitakazotolewa katika sekta Usafirishaji, Ujenzi na Mawasiliano. Maelezo ya programu hizo ni kama ifuatavyo:

### G.2.1 PROGRAMU YA USAFIRISHAJI.

**110. Mheshimiwa Spika,** matokeo ya programu hii ni kuwepo kwa miundombinu na huduma za usafiri zilizo bora, salama na endelevu. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu ya Usafirishaji itakuwa na programu ndogo moja ambayo ni; Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji.

#### G.2.1.1 Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji

**111. Mheshimiwa Spika,** programu hii ndogo inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Wakala wa Barabara Zanzibar pamoja na Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar. Programu hii ina lengo la kuhakikisha huduma bora za usafiri zilizo salama zinapatikana muda wote Unguja na Pemba. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara kupitia Taasisi zinazosimamia programu hii, imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

## IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

**112. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia programu ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji imepanga kuendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ifuatayo:-

i. Kuendelea na Ujenzi wa barabara kuu Unguja na Pemba; Ikiwemo ujenzi wa Barabara ya Chake - Wete 22.1 km, Tunguu – Makunduchi 48 km , Fumba – Kisauni 12 km, Chake – Mkoani 43.5 km, Barabara ya Bumbwini – Pangatupu- Mahonda 7.1 km, Mangapwani – Zingwezingwe, Mfenesini – Mangapwani 7 km, Kizimbani – Kiboje 7.2 km na Barabara ya Regeza Mwendo - Mwakaje – Mfenesini 14 km, Kitogani – Paje 11.9 km, Barabara ya Tumbatu kuanzia (Jongoe hadi Mwana wa Mwana Mnarani) 9km.

ii. Kuendelea na Ujenzi wa Barabara za ndani zenye urefu wa kilomita 275.9 Unguja na Pemba,

iii. Kuendelea na Ujenzi wa barabara za Mjini Unguja zenye urefu wa kilomita 100.9.

iv. Kuimarisha Uwanja wa Ndege wa Pemba kwa kuongeza urefu wa barabara ya kutua na kurukia ndege, njia ya kupitia ndege pamoja na maegesho ya ndege (runway, taxi way and apron), kujenga jengo jipya la abiria (Terminal Building) na miundombinu husika itakayowezesha uwanja huo kutua ndege aina ya Code C (Boeing 737-800) na zinazolingana.

v. Kujenga jengo la abiria Terminal II pamoja na kuanza maandalizi ya ujenzi wa jengo la abiria la Terminal IV katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa AAKIA.

vi. Kuanza ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani pamoja na kuendelea kuweka miundombinu katika eneo la bandari hiyo.

vii. Kujenga Bandari mpya kisasa ya Abiria Maruhubi pamoja na

viii. Kununua boti mbili za abiria za mwendokasi zitakazotoa huduma ya kusafirisha abiria baina ya Visiwa vya Unguja,Pemba, Dar es Salaam, Tanga na Mombasa, Kenya.

**113. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imepanga kutumia jumla ya T**SH 1,065,216,174,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo Unguja na Pemba, ikiwa **TSH 572,943,683,000** ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na **TSH 492,272,491,000** ni mchango kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**WAKALA WA BARABARA ZANZIBAR**

**114.Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wakala wa Barabara Zanzibar kupitia programu ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji imepanga kuzifanyia matengenezo barabara mbalimbali Unguja na Pemba ikiwemo barabara ya Selem - Mbuzini km 3, barabara ya Kisauni - Mbuyuni km 0.7, barabara ya Langoni - Maeneo huru 3.5km, kukamilisha ujenzi wa barabara ya Mgelema - Wambaa km 4 kwa kiwango cha lami pamoja na Barabara ya Chanjaani – Pujini km 5 kwa kiwango cha kifusi. Pia Wakala imepanga kuifanyia matengenezo Barabara ya Wete – Gando na Wete – Konde kwa urefu wa kilomita 5. Aidha kwa upande wa Matengenezo ya kawaida. Wakala wa Barabara imepanga kuzifanyia matengenezo ya barabara za lami kilomita 369.9 kwa Unguja na kilomita 201.95 kwa Pemba. **Kiambatanisho Nambari 11 kinahusika.**

**115. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa kazi za kawaida Wakala imepanga kuendelea kutekeleza shughuli za kiutumishi na utawala kwa kununua vifaa mbalimbali vya Ofisi pamoja kuweka mazingira mazuri ya kazi. Pia, Wakala imepanga kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu Wafanyakazi 50 ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi.

**116.Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wakala wa Barabara Zanzibar imepangiwa kutumia jumla ya **TSH 23,723,100,000** ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini kwa kazi za kawaida na matengenezo ya Barabara Unguja na Pemba. Kati ya fedha hizo **TSH 679,200,000** ni matumizi mengineyo, **TSH 5,043,900,000** ni mshahara na **TSH 18,000,000,000** ni kwa ajili ya matengenezo ya barabara.

## WAKALA WA KARAKANA KUU YA MAGARI ZANZIBAR

**117. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar imepanga kutekeleza mambo yafuatayo:-

i. Kufanya matengenezo ya gari 2,300 za Serikali na binafsi pamoja na kutoa Ushauri wa kitaalamu wa ununuzi na uuzaji wa magari hadi kufikia taasisi 40.
ii. Kuandaa mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kurahisisha utoaji na upatikanaji wa huduma na taarifa zinazohusiana na kazi za Wakala.
iii. Kuimarisha Ofisi za Wakala na Karakana zake kwa Kuzifanyia matengenezo madogo madogo zana, majengo na miundombinu mengine pamoja na kuendelea kuwapatia wafanyakazi sita (6) mafunzo ya muda mrefu na wafanyakazi 13 mafunzo ya muda mfupi ili waweze kutoa huduma bora kwa jamii.

**118. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha, 2024/2025 Wakala wa Karakana imepangiwa kutumia jumla ya **TSH 2,875,900,000** ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo **TSH 894,100,000** ni matumizi mengineyo na **TSH 1,981,800,000,** ni ruzuku ya mshahara.

**119. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji inaombewa kutumia jumla ya **TSH 1,092,041,074,000** kwa kazi za kawaida, Ruzuku na miradi ya maendeleo kwa taasisi zinazosimamia programu hii.

## G.2.2. PROGRAMU YA UJENZI NA MAJENGO YA SERIKALI

**120. Mheshimiwa Spika,** matokeo ya programu hii ni kuwepo kwa usimamizi imara wa ujenzi na majengo bora ya Serikali na binafsi yaliyo salama na yenye viwango vinavyokubalika kwa mujibu wa miongozo iliyopo na yenye kukidhi mahitaji ya watumiaji wote. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 programu hii itakuwa na programu ndogo moja ambayo ni; Usimamizi wa Ujenzi na Majengo ya Serikali.

**G.2.2.1. Programu ndogo ya Usimamizi wa Ujenzi na Majengo ya Serikali.**

**121. Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Wakala wa Majengo na ina lengo la kuhakikisha kuwepo kwa usimamizi imara wa ujenzi na majengo bora ya Serikali na binafsi na yaliyo salama.

Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wakala wa Majengo kupitia programu hii imepanga kuendelea kutoa huduma za Ushauri Elekezi kwa miradi mbali mbali ya ujenzi wa majengo ya Serikali, kuandaa nyaraka za ujenzi na BoQ 32, kati ya nyaraka hizo, 20 zitaandaliwa kwa upande Unguja na 12 zitaandaliwa kwa upande Pemba. Pia Wakala imepanga kusimamia miradi 45 ya ujenzi, kati ya miradi hiyo 30 itasimamiwa Unguja na 15 itasimamiwa Pemba. Aidha, Wakala wa Majengo kwa kushirikina na Wizara imepanga kukamilisha mchakato wa uandaaji wa Sheria ya Wakala wa Majengo pamoja na Mpango Mkakati wa Wakala (Strategic Plan) wa kipindi cha miaka mitano ijayo.

**122. Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Majengo Zanzibar imepanga kuandaa ramani na makisio ya gharama za ujenzi wa nyumba za makaazi ya Makamu wa Kwanza na Makamu wa Pili wa Rais, kuandaa makisio ya gharama za ujenzi wa nyumba arobaini (40) za viongozi wa Serikali (Mawaziri, Makatibu Wakuu na wengine wenye sifa za kupatiwa nyumba za makaazi kwa nafasi wanazozitumikia) katika eneo la Mazizini pamoja na ramani na makisio ya gharama za ujenzi wa majengo mawili (2) ya Afisi za Serikali yatakayojumuisha taasisi zaidi ya moja Unguja na Pemba. Majengo hayo yatajengwa katika maeneo ya Mazizini kwa Unguja na Pemba katika maeneo ya Chake Chake.

**123. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha, 2024/2025 Wakala wa Majengo imepangiwa kutumia jumla ya **TSH 2,795,300,000** ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo **TSH 750,000,000** ni matumizi mengineyo na **TSH 2,045,300,000** ni ruzuku ya mshahara.

**124. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu ndogo ya Usimamizi wa Ujenzi na Majengo ya Serikali inaombewa kutumia jumla ya TSH 2,869,400,000 kwa kazi za kawaida na Ruzuku kwa taasisi zinazosimamia programu hii.

## G.2.3 PROGRAMU YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA).

**125. Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya programu hii ni kuwepo kwa miundombinu na huduma bora na salama za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 programu hii ina programu ndogo moja ambayo ni; Miundombinu na Huduma za TEHAMA.

### G.2.3.1 Programu Ndogo ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA

**126. Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Idara ya Mawasiliano na ina lengo la kuhakikisha kuwepo kwa miundombinu na huduma bora za TEHAMA zilizo salama na endelevu pamoja na kushajihisha Ubunifu na Uchumi wa Kidijitali kwa kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji yanayotokana na uwekaji wa Sera na Sheria rafiki. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Idara ya Mawasiliano kupitia programu hii imepanga kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuweka mazingira wezeshi kwa kuimarisha Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na kuvutia wawekezaji kwa kuweka Sera, Sheria na kanuni rafiki, (Digital Ecosystem).
ii. Kuimarisha miundombinu ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa Jamii ya Zanzibar pamoja na kuimarisha usalama wa mitandao (Digital Data Center, Digital services, Connectivity and Cyber Security).
iii. Kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma za kiserikali na binafsi kwa kutumia mifumo ya Kidijitali kwa wananchi (Information Systems).
iv. Kuibua vipaji na kuimarisha ubunifu katika Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa lengo la kupata maarifa na ujuzi utakao

jenga ubobezi kwa vijana na kuongeza soko la ajira kupitia TEHAMA (Digital Innovation and Enterprenuership).

v. Kushajihisha matumizi na kuboresha mfumo wa anuani za makaazi Zanzibar (Engagement with Community).

vi. Kuendelea kuwajengea uwezo wananchi 4,000 kwa kuwapatia mafunzo ya kidigitali kupitia vituo vya TEHAMA jamii.

**127. Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza malengo hayo, Wizara kupitia Idara ya Mawasiliano imejipanga kuchukua hatua za msingi za kushirikiana na wadau wa maendeleo katika Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ili kupata nguvu ya pamoja ya kutekeleza malengo ya maendeleo endelevu ya mwaka 2030. Vilevile, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2050 imebainisha na kutoa kipaumbele kwa sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kuwa ndio sekta wezeshi kufikia malengo ya Dira ya Zanzibar 2050 ya uchumi wa kidijitali.

**128. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu Ndogo ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA inaombewa kutumia jumla ya **TSH 6,687,907,000** kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo. Kati ya fedha hizo, **TSH 400,700,000** ni matumizi mengineyo, **TSH 287,207,000** ni mshahara na **TSH 6,000,000,000** kwa ajili ya kazi za maendeleo.

## G.2.4 PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA

**129. Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya programu hii ni kuwepo kwa uratibu wa Shughuli za Wizara, Sera, Mipango ya kisekta pamoja na usimamizi mzuri wa rasilimali watu. Programu hii ina programu ndogo tatu (3) ambazo ni; Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji, Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara pamoja na Uratibu wa shughuli za Wizara Pemba.

### G.2.4.1. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji

**130. Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi na ina lengo la kuimarisha huduma za ofisi na usimamizi wa rasilimali watu katika Wizara.

**131. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Idara ya Uendeshaji na Utumishi kupitia programu hii itaendelea kutekeleza masuala ya kiutumishi na Uendeshaji wa Wizara ikiwemo kuweka mazingira mazuri ya kazi, kusimamia maslahi ya watumishi, kununua vitendea kazi ili kuongeza ufanisi wa kazi. Vilevile, Idara imepanga kutoa Makala na machapisho mbalimbali kuhusu utekelezaji wa shughuli na mafanikio ya Wizara. Pia Idara imepanga kuufanyia mapitio na kuandaa mkataba wa huduma kwa Umma pamoja na kufanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo katika sekta za Wizara.

**132. Mheshimiwa Spika,** ili kuongezea ujuzi, ufanisi na tija kwa wafanyakazi wa Wizara, Idara imepanga kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi wafanyakazi 50 wa Wizara Unguja na Pemba kwa mujibu wa mpango wa mafunzo wa Wizara.

**133. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji inaombewa kutumia jumla ya **TSH 3,376,262,000** kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, TSH 1,822,862,000 ni mshahara na **TSH 1,553,400,000** ni kwa matumizi mengineyo.

### G.2.4.2 Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara

**134. Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na ina lengo la kuhakikisha Mipango na Sera mbalimbali za Sekta ya Usafirishaji, Ujenzi na Mawasiliano zinatayarishwa pamoja na kufuatilia utekelezaji wake.

**135. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia programu hii imepanga kuendelea kuratibu na kufuatilia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kutayarisha muongozo wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa kazi za Wizara, kutoa mafunzo ya utayarishaji wa bajeti kwa watendaji wa Wizara kulingana na miongozo kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango inayotolewa kila mwaka, kuratibu na kufanya tafiti

zinazohusu Sekta ya Usafirishaji na Mawasiliano, kuendelea kufanya utafiti juu ya mfumo wa Usafiri Zanzibar utakaotoa mwelekeo wa namna ya kutayarisha Sera bora ya Usafiri pamoja na Mpango Mpya wa Usafiri Zanzibar (Zanzibar Transport Master Plan). Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa kushirikiana na Idara ya Mawasiliano itaendelea kukamilisha Sera ya Kidigitali itakayojumuisha masuala ya TEHAMA. Vilevile, Idara itaendelea kukusanya na kuchambua takwimu za maendeleo ya sekta na kuweka mpango bora wa utunzaji wa kumbukumbu za takwimu.

136. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imepanga kutayarisha na kuratibu mapitio ya Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali inayosimamia Sekta ya Ujenzi, Usafirishaji na Mawasiliano kwa kuzifanyia marekebisho ili ziendane na mahitaji na mabadiliko yaliyopo kwa sasa. Pia, Idara itaendelea kuratibu mashirikiano ya kisekta baina ya Taasisi za ndani na nje ya nchi ya kikanda na Kimataifa ikiwemo vikao vya mashirikiano baina ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi (SMZ), Wizara ya Ujenzi (SJMT), Wizara ya Uchukuzi (SJMT) pamoja na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (SJMT). Vilevile, Idara itaendelea kuratibu Taasisi na Mashirika yanayojitegemea yaliyo chini ya Wizara hii.

137. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara inaombewa kutumia jumla ya **TSH 886,739,000** kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizio, **TSH 352,439,000** ni mshahara na **TSH 534,300,000** ni matumizi mengineo.

### G.2.4.3 Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba

138. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Ofisi Kuu Pemba na ina lengo la kuhakikisha majukumu ya Wizara yanatekelezwa ipasavyo kwa upande wa Pemba.

139. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi Kuu Pemba imepanga kutekeleza kazi zake kama ifuatavyo; kuratibu na kusimamia maslahi ya wafanyakazi, kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda

mfupi wafanyakazi, kufanya matengenezo ya Jengo la Ofisi pamoja na kusimamia upatikanaji wa huduma muhimu za uendeshaji wa Ofisi.

Pia, Ofisi Kuu - Pemba itaendelea kufanya ufuatiliaji na kusimamia kazi za miradi mbali mbali ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara ikiwemo Ujenzi wa Barabara za Ndani na Barabara Kuu, uimarishaji wa Uwanja wa Ndege wa Pemba pamoja na miradi mengine inayotekelezwa na Wizara kwa upande wa Pemba.

Vilevile, Ofisi kuu Pemba itaendelea kutoa elimu ya TEHAMA kupitia vituo vya TEHAMA jamii kwa wananchi, kuratibu na kuendeleza matumizi ya Anuani za Makaazi na Postikodi pamoja na kuendelea kusimamia miundombinu ya TEHAMA.

**140. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba inaombewa kutumia jumla ya **TSH 1,262,492,000** kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, **TSH 762,492,000** ni mshahara n**a TSH 500,000,000** ni kwa matumizi mengineyo.

## H. HITIMISHO

**141. Mheshimiwa Spika,** kabla sijamaliza hotuba yangu hii sina budi kutoa shukurani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu na ustahamilivu wakati wote nilipokua nikitoa maelezo ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi. Ni matumaini yangu kwamba Baraza lako Tukufu litatoa michango ambayo itasaidia Wizara kuendelea kutekeleza majukumu yake ipasavyo ya kuwahudumia wananchi wetu na hatimae kuipitisha Bajeti hii kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara zilizopangwa katika kila programu kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**142. Mheshimiwa Spika,** Pia naomba nichukue fursa hii kwa mara nyengine tena kumshukuru sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa moyo wake wa kupenda Amani na Maendeleo kwa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Namuomba Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema yeye na familia yake ili aendelee kutuongoza kwa mafanikio makubwa.

**143. Mheshimiwa Spika,** mafanikio ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ambayo nimeyaeleza kwa kina katika hotuba hii, ni matokeo ya ushirikiano wa wadau mbalimbali wa ndani na nje ya Nchi. Kwa niaba ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, napenda kuchukua fursa hii kuzitambua, kuzishukuru na kuzipongeza Taasisi mbalimbali tulizoshirikiana nazo katika kuendeleza Sekta mbalimbali za Wizara hii. Shukurani za dhati ziende kwa Washirika wa Maendeleo wakiwemo Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi Afrika (BADEA), Saudi Fund, United Kingdom Export Finance ya Uingereza na Mashirika ya Umoja wa Mataifa yakiwemo IMO, ICAO, ITU na UNCDF.

**144. Mheshimiwa Spika,** vile vile, natoa shukurani zangu kwa Taasisi binafsi zinazotoa huduma za mawasiliano na usafirishaji hapa Zanzibar ikiwemo Kampuni za mawasiliano za TigoZantel, Halotel, Airtel, Vodacom, TTCL na Zanlink. Kwa upande wa Kampuni za usafirishaji wa baharini tunazipongeza Kampuni za African Shipping Corporation, Zanzibar Shipping Corporation, Kilimajaro Fast Ferries Marine Services Limited, Azam Marine Company LTD, Zan Fast Ferries, Ikraam Sealine Company pamoja na Kampuni ya Danaos inayotoa ajira ya ubaharia kwa wananchi wa Zanzibar.

Kwa upande wa usafiri wa anga tunazipongeza Kampuni za Air Tanzania, Assalam Air, Costal Travel, Auric Air, Unity Air, Pelican Air, Precision Air, Zan Air, Regional Air, Flight link, My Fly Aviation, Safari Air Link, Air Excel, Tropical Air, Fly Zanzibar na Kampuni za Kimataifa ikiwemo Ethiopian Airlines, Euro wings, Lufthansa Airline, Turkish Airlines, Blue Panorama, Qatar Airlines, Fly Dubai, Air France, Kenya Airways, Global Airways, Oman Air, Uganda Air, Israil Airlines, KLM Airlines, 540 Aviation, Air Kenya na nyenginezo.

Kwa upande wa Usafiri wa nchi kavu tunawapongeza na kuwashukuru wamiliki na watendaji wa vyombo vya usafiri wa nchi kavu ikiwemo Daladala, Magari ya Shamba, Bodaboda pamoja na Bajaji kwa mchango wao mkubwa wanaoutoa katika kufanikisha huduma za usafiri kwa wananchi.

Kwa upande wa Sekta ya Ujenzi, tunazipongeza Kampuni mbalimbali za ujenzi zinazofanya kazi Zanzibar pamoja na kuwashukuru wataalamu wa ujenzi waliopo Zanzibar kwa mchango wao mkubwa katika kuleta maendeleo ya nchi yetu.

**145. Mheshimiwa Spika,** Kampuni hizi zimechangia kwa kiasi kikubwa katika kuimarisha Sekta ya Usafirishaji, Ujenzi na Mawasiliano hapa Zanzibar. Kwa niaba ya Serikali na kwa kupitia Baraza lako Tukufu noamba kutoa wito, kuwaomba wadau waliotajwa hapo juu na wengineo kuendelea kushirikiana na Serikali katika kutoa huduma za usafirishaji, ujenzi na mawasiliano hapa chini.

**146. Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati viongozi wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi nikianza na Mheshimiwa Nadir Abdulatif Alwardy Naibu Waziri ambae pia ni Mwakilishi wa kuchaguliwa na wananchi katika Jimbo la Chaani, Dkt. Mngereza Mzee Miraji Katibu Mkuu, Ndugu Makame Machano Haji Naibu Katibu Mkuu - Ujenzi na Uchukuzi, Dkt. Mzee Suleiman Mndewa Naibu Katibu Mkuu - Mawasiliano, Ndugu Ibrahim Saleh Juma Afisa Mdhamini, Ndugu Mahfoudh M. Hassan Mkurugenzi Idara ya Uendeshaji na Utumishi, na Wakurugenzi Wakuu wa Mashirika nikianza na Ndugu Akif Ali Khamis Mkurugenzi Mkuu Shirika la Bandari, Ndugu Seif A. Juma Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, Ndugu Sheikha A. Mohamed Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Usafiri Baharini, Ndugu Haji A. Zubeir Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani, Eng. Shukuru A. Suleiman Mkurugenzi Mkuu Shirika la Mawasiliano, Eng. Cosmas M. Masolwa Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Wakala wa Barabara, Eng. Kassim A. Omar Mkurugenzi Mtendaji Wakala wa Majengo, Eng. Makame H. Makame Mkurugenzi Muendeshaji Shirika la Meli, Ndugu Hussein A. Hussein Mkurugenzi Mtendaji Wakala wa Karakana Kuu ya Magari hii pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa ushirikiano na juhudi wanazozichukua katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa.

**147. Mheshimiwa Spika,** naomba pia nitoe shukurani zangu za dhati na za kipekee kwa familia yangu kwa kuniunga mkono na kunipa moyo muda wote nikiwa katika kutekeleza majukumu yangu ya kikazi.

**148.Mheshimiwa Spika,** ni matumaini yangu kwamba maelezo niliyoyatoa katika hotuba hii ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi yanatosha katika kuliarifu Baraza lako Tukufu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika kipindi kilichopita na mpango wa utekelezaji wa majukumu kwa kipindi kijacho cha mwaka wa fedha 2024/2025. Hivyo, ni matumaini yangu kwamba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wataichangia hotuba hii ipasavyo.

## I. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025.

**149. Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni ya kuiwezesha Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kutekeleza majukumu na malengo yake yaliyoainishwa katika Programu Kuu nne (4) katika hotuba hii pamoja na utekelezaji wa Ilani Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 -2025, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **TSH 1,107,123,874,000** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na maendeleo ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**150. Mheshimiwa Spika,** kati ya fedha hizo, **TSH 35,907,700,000** ni kwa ajili ya kazi za kawaida (**TSH 3,225,000,000** ni mshahara, **TSH 3,288,400,000** ni matumizi mengineyo na **TSH 29,394,300,000** ni Ruzuku), **TSH 572,943,683,000** ni mkopo kutoka kwa Washirika wa maendeleo na **TSH 498,272,491,000** ni fedha kutoka Serikalini kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**151. Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu kuruhusu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kukusanya mapato ya **TSH 3,792,926,000** kutokana na vianzio mbalimbali vilivyomo ndani ya Wizara hii kwa mwaka 2024/2025.

**152. Mheshimiwa Spika,** kwa heshima kubwa nawaomba Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waipokee, waijadili, watushauri, watuelekeze na baadae watupitishie Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**153. Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja.

....................................

**Dkt. Khalid S. MOHAMED (MBM)**
**WAZIRI WA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI**

**VIAMBATANISHO**

**Kiambatanisho Nambari 1A: Fedha za Matumizi ya Kawaida Na Maendeleo Kwa Programu Kwa Kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024.**

| Nam. | Programu Kuu/ Programu Ndogo | Makadirio kwa mwaka 2023/2024 | Makadirio kwa Kipindi cha Julai 2023 – Machi 2024 | Matumizi Halisi Julai 2023 hadi Machi 2024 | Asilimia ya Fedha iliyopatika na kwa miezi tisa | Asilimia ya Fedha iliyopatikan a kwa mwaka |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **1** | **Programu ya Usafirishaji** | | | | | |
| 1.1 | Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji | 560,208,700,000 | 464,452,878,828 | 349,899,663,639 | 75.3 | 62.3 |
| | **Jumla ya Programu Kuu** | **560,208,700,000** | **464,452,878,828** | **349,899,663,639** | **75.3** | **62.3** |
| **2** | **Programu ya Ujenzi na Majengo ya Serikali** | | | | | |
| **2.1** | Usimamizi wa Ujenzi na Majengo ya Serikali. | - | - | 205,500,509 | - | - |
| | **Jumla ya Programu Kuu** | **-** | **-** | **205,500,509** | **33** | **23** |
| **3** | **Programu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)** | | | | | |
| 3.1 | Miundombinu na Huduma za TEHAMA | 6,599,771,000 | 5,947,589,847 | 1,719,175,594 | 29 | 26 |
| | **Jumla ya Programu Kuu** | **6,599,771,000** | **5,947,589,847** | **1,719,175,594** | **29** | **26** |
| **4** | **Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi** | | | | | |
| 4.1 | Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji | 2,760,140,000 | 2,005,716,393 | 2,778,415,771 | 139 | 101 |
| 4.2 | Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara | 922,308,000 | 790,577,500 | 522,285,588 | 66 | 57 |
| 4.3 | Uratibu wa Shughuli za Wizara – Pemba | 999,781,000 | 930,360,112 | 656,950,920 | 71 | 53 |
| | **Jumla ya Programu Kuu** | **4,682,229,000** | **3,726,654,005** | **3,957,652,279** | **106** | **81** |
| | **Jumla Kuu ya Programu Kuu za Wizara** | **571,490,700,000** | **474,127,122,680** | **355,781,992,022** | **75** | **62** |

## Kiambatanisho Nambari 1B: Fedha Zilizopatikana kwa Kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024

| Nam. | Maelezo | Bajeti kwa mwaka 2023/2024 | Bajeti kwa kipindi cha Julai 2023 – Machi, 2024 | Fedha iliyopatikana kwa kipindi cha Julai 2023 – Machi, 2024 | Asilimia ya Fedha iliyopatikana kwa Julai 2023 – Machi, 2024 | Asilimia ya Fedha iliypatika na kwa mwaka |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mshahara | 2,751,300,000 | 2,063,475,749 | 3,008,056,086 | 145.7 | 109.3 |
| 2 | Ruzuku ya Mshahara | 5,766,200,000 | 4,629,360,028 | 4,616,835,925 | 99.7 | 73 |
| 3 | Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi (OC) | 2,630,700,000 | 2,210,768,103 | 1,248,363,100 | 56.5 | 47 |
| 4 | Ruzuku ya Uendeshaji wa Ofisi (OC) | 895,500,000 | 663,518,800 | 694,992,796.39 | 104.7 | 36 |
| 5 | Fedha za miradi ya Maendeleo (SMZ) | 235,447,000,000 | 188,560,000,000 | 196,552,438,365.8 | 104 | 83 |
| 6 | Fedha za Miradi kwa Washirika wa Maendeleo | 324,000,000,000 | 276,000,000,000 | 149,661,305,748.6 | 54 | 46 |
| | **JUMLA KUU** | **571,490,700,000** | **474,127,122,680** | **355,781,992,021** | **75** | **62** |

**Kiambatanisho Nambari 2. Matengenezo ya Vyombo vya Moto kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024.**

| **Nam** | **Vyombo vya moto** | **Unguja** | | | | | **Pemba** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Shabaha | | Utekelezaji miezi tisa | Asilimia % | | Shabaha | | Utekelezaji miezi tsia | Asilimia % | |
| | | Mwaka | Miezi tisa | | Miezi tisa | Mwaka | Mwaka | Miezi tisa | | Miezi tisa | Mwaka |
| 1 | Magari ya Serikali | 1,400 | 1,050 | 1,161 | 110.6 | 82.9 | 420 | 315 | 111 | 35.2 | 26.4 |
| 2 | Magari binafsi | 200 | 150 | 93 | 62 | 46.5 | 60 | 45 | 5 | 11.1 | 8.3 |
| | **Jumla** | **1,600** | **1,200** | **1,254** | **104.5** | **78.4** | **480** | **360** | **116** | **32.2** | **24.2** |

**Kiambatanisho Nambari 3A: Orodha ya Barabara zilizofanyiwa Usafi wa Ukataji Majani, Usafishaji Msingi na Makalvati kwa Unguja na Pemba**

**UNGUJA**

| | Jina la barabara | Urefu (km) |
|---|---|---|
| **1** | Kibuteni - Kizimkazi Dimbani na Mkunguni | 4 |
| **2** | Kibuteni – Makunduchi Pwani | 4 |
| **3** | Kibele Dr. Shein Road | 2 |
| **4** | U/Kaebona - Jozani | 6 |
| **5** | Tunguu -Bungi – Kikungwi | 5 |
| **6** | Tangi la Maji – Mtende | 4 |
| **7** | Mshelishelini – P/Mchangani | 7.5 |
| **8** | Matemwe - Muyuni | 7.5 |
| **9** | Pongwe - Matemwe | 26.29 |
| 10 | Bububu - Mndo | 3.94 |
| 11 | Sharifumsa- Mwanyanya-Bububu school | 3.80 |
| 12 | Kwanyanya-Mkanyageni | 3.08 |
| 13 | Kitundu-Ndagaa | 5.50 |
| 14 | Regezamwendo-Mfenesini | 14.27 |
| 15 | Koani - Machui - Kitumba | 5.50 |
| 16 | Kidimni- Kitope | 19.00 |
| 17 | Koani-Jumbi | 6.30 |
| 18 | Pongwe - Matemwe | 20.40 |
| 19 | Mkwajuni - Nungwi | 19.00 |
| 20 | Upenja - Kiwengwa | 8.31 |
| 21 | Tunguu- Upenja-Kinyasini | 26.76 |
| 22 | Dunga-Chwaka | 14.42 |
| 23 | Kipilipilini - Pongwe | 14.00 |
| 24 | Jendele-Cheju-Kaebona | 12.00 |
| 25 | Donge-Muwanda | 4.00 |
| 26 | Mahonda-Kinyasini-Mkokotoni | 15.00 |
| 27 | Kitope-Kinduni | 3.80 |

| | Jina la barabara | Urefu (km) |
|---|---|---|
| 28 | Pale-Kiongele | 4.61 |
| 29 | Njianne - Bambi | 6.50 |
| 30 | Kwakibawa - Umbuji | 5.10 |
| 31 | Mfenesini-Bumbwini (Amani-Dunga) | 11.82 |
| 32 | Bububu Police station - Kwanyanya | 2.80 |
| 33 | Kwanyanya - Mahonda | 17.00 |
| 34 | Paje - Michamvi | 17.82 |
| 35 | Paje - Makunduchi | 17.30 |
| 36 | Kitogani - Paje | 11.60 |
| 37 | Fuoni-Kombeni | 8.58 |
| | **Jumla Unguja** | **368.50** |

**PEMBA**

| Nam | Jina la barabara | Urefu (km) |
|---|---|---|
| 1 | Mkoani port - Makombeni | 4.2 |
| 2 | Kilindi – Micheweni | 5 |
| 3 | Mkanyageni – shidi | 2.2 |
| 4 | Meli tano - Madenjani | 13.5 |
| 5 | Chwale – Likoni | 1.9 |
| 6 | Mgagadu – Kiwani | 7.5 |
| 7 | Mtambile - Mwambe | 9.4 |
| 8 | Mtambile - Kangani | 4.8 |
| 9 | Mzingani -Wambaa | 11.7 |
| 10 | Chanjamjawiri -Tundauwa | 11.9 |
| 11 | Kenya - Chambani | 3.4 |
| 12 | Chanjaani - Pujini | 5.5 |
| 13 | Ole -Kengeja | 35 |
| 14 | Chanjaani - Mbuguani | 27.5 |
| 15 | Mtuhaliwa - Chokocho | 8.8 |
| 16 | Bahanasa -Uondwe | 10.35 |
| 17 | Chanjaani - M/mane | 2.91 |
| 18 | M/Takao –M/Karim | 13.44 |
| | **Jumla Pemba** | **179** |

**Kiambatanisho Nambari 3B: Orodha ya Barabara zilizofanyiwa Matengenezo ya kawaida ya Uzibaji wa Mashimo.**

| Nam. | Jina la Barabara | Mita za Mraba |
|---|---|---|
| | **Unguja** | |
| 1 | Mwembebeni – Mikunguni | 564 |
| 2 | Nyumbambili – Mwanakwerekwe C | 707 |
| 3 | Michenzani – Mkunazini – Malindi | 604 |
| 4 | Dunga – Chwaka | 1024 |
| 5 | Mshelishelini – Pwani Mchangani | 360 |
| 6 | Amani – Mwera | 630 |
| 7 | Mahonda – Donge | 900 |
| 8 | **Jumla Unguja** | **4,789** |
| | **Pemba** | |
| 1 | Ole – Kengeja | 40 |
| 2 | Airport – Chanjaani | 80 |
| 3 | Machomanne – Vitongoji | 1200 |
